**OrODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 19 Juni, 2015**

*(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe katika Mkutano wa 18 wa Baraza la Nane la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 21 Januari 2015 hadi 30 Januari 2015 Baraza lilipitisha Miswada Minne ya Sheria kama ifuatayo:

(1) Sheria ya Kuanzisha sheria za kupunguza na kukabiliana na Maafa Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.

(2) Mswada wa Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar na Mambo yanayohusiana na hayo.

(3) Sheria ya Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo endelevu namba 2 ya mwaka 1996 na kuweka badala yake masharti bora ya kuhifadhi, kulinda na kusimamia mazingira Zanzibar na Mambo yanayohusiana na hayo.

(4) Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na Mambo yanayohusiana na hayo.

Katika Miswada hiyo minne, miswada mitatu ya mwanzo imeshatolewa taarifa yake itakuwa tayari na imesainiwa na Mhe. Rais, hivyo imekuwa sheria kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 91(3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012. Naomba kutoa taarifa rasmi kwamba Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na Mambo yanayohusiana na hayo sasa umesainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na kuwa Sheria kamili. Kwa hivyo, naomba kutoa taarifa hiyo kwamba na mswada huu wa Maadili ya Viongozi tayari umekuwa sheria kamili, baada ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuweka saini. Naomba kuwasilisha.

Katibu tuendelee. (*Makofi*)

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa Mwaka 2015/16

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe jana tulipoondokeana hapa tulikuwa tumemaliza wachangiaji na nilikuwa sina hata mmoja, kwa maana hiyo namwita sasa hivi Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kuchangia. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia asubuhi hii tukaweza kufika hapa kutekeleza majukumu yetu tukiwa ni viongozi kama ambavyo tumeagizwa na wananchi.

Mhe. Naibu Spika, pia niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kutusaidia sana katika miongozo na zaidi Kamati ile ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa miongozo yao muda wote wakati tukifanya nao kazi.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote lakini nataka nichukue fursa hii asubuhi ya leo kumpongeza sana Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kitendo alichokifanya jana; cha kujitokeza kuchukua fomu ya kugombea na kuwania tena nafasi ya Urais wa Zanzibar. Nampongeza sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, wakati tukifanya kazi na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo tumefanya kazi kwa vizuri, na ndio maana jana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Hija Hassan Hija nichukue nafasi hii kumpongeza kwa jinsi alivyosaidia sana katika kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya changamoto ambazo Waheshimiwa Wajumbe wamezitoa hapa Barazani.

Mhe. Naibu Spika, kati ya mengi yaliyojitokeza Wajumbe 14 wa Baraza lako hili wamechangia, ambapo Mhe. Viwe Khamis Abdalla ndiye aliyewasilisha kwa niaba ya Kamati. Mhe. Waziri atakapokuja hapa atawataja wote hao kwa majina. Mimi nitazungumzia yale ya jumla ambayo yamejitokeza miongoni mwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, suala zima la tenda iliyotoleshwa katika gazeti na Katibu Mkuu wa Wizara kuhusiana na duka la vioo.

Mhe. Naibu Spika, duka hili liko chini ya Serikali kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, na duka hili limegawika sehemu mbili. Kuna sehemu

ambayo inatumiwa na masonara ambayo sehemu hii masonara hawa walikabidhiwa na mwenyewe Rais wa Kwanza na Muasisi wa Taifa letu la Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Aman Karume ili wafanyie shughuli zao. Kwa maana hiyo sisi kama wizara kuna taratibu ambazo tunatakiwa tuzipitie kwa kukaa nao pamoja na hatimaye tuweze kufikia muafaka na masonara hawa.

Mhe. Naibu Spika, lakini sehemu ya pili ndiyo iliyokodishwa na ndiyo ambayo hasa imetolewa tenda. Sehemu hiyo kwa sasa kama nilivyojibu katika swali namba 69, swali pekee tuliloletewa katika wizara yetu katika kipindi kizima hichi cha bajeti, ambalo nilijibu tarehe 21/5/2015 naomba nirejee hapa kwamba tenda zile zipo wizarani, na utaratibu unaendelea kushughulikiwa. Lakini vile vile tukizingatia kwamba kuna programu kubwa ya serikali iliyoshtushwa kama ambavyo nimejibu katika suala lile. Programu ile ya maendeleo ya kuendeleza eneo lote la Darajani.

Sasa tukizingatia mpango ule lakini pia tukisubiri taratibu za kufungua tenda zikamilike, basi niwaombe Waheshimiwa waliochangia suala hili taratibu hizi zikikamilika tenda hizo zitafunguliwa *in shaa Allah* patakapokuwa na majaaliwa na tukiwa wazima.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine lililojitokeza katika Baraza lako ni suala zima la upandaji wa bei za vyakula. Sote tunafahamu kwamba mtiririko mzima wa bei si za vyakula tu lakini bidhaa takriban zote unasukumwa kwa kiasi kikubwa na kupanda au kushuka kwa dola. Hivi karibuni tumeshuhudia dola ikipanda kwa kiasi kikubwa sana, na ndio sababu kubwa iliyopelekea kupanda kwa bei za vyakula.

Mhe. Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wakubaliane na mimi kwamba suala la upandaji wa dola ni suala la ulimwengu mzima, na kwa kiasi kikubwa kuli- *control* sisi hapa Zanzibar si rahisi, lakini bado kama wizara tutaendelea kukaa na wafanyabiashara. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe waliozungumzia suala hilo basi wawe na subira, kwa saabbu upandaji huu wa dola kwa kweli umeathiri wananchi kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini suala jengine lililozungumzwa katika Baraza lako ni suala la Shirika la Viwango la Zanzibar. Shirika hili tunafahamu sheria yake ilipitishwa hapa Barazani hivi karibuni tu. Kwa hiyo, kuna taratibu nyingi ambazo zinatakiwa kukamilishwa ili hatimaye Shirika hili liweze kufanya kazi kama ambavyo tumetarajia.

Mhe. Naibu Spika, lakini katika kufanyia kazi Shirika hili, imebainika kwamba mpaka hapa litakapokuwa shirika kamili linaweza kujitegemea ni kiwango

kikubwa cha fedha ambazo zinahitajika takriban pesa za Kitanzania ni bilioni sita, lakini tukichanganya na maabara zake, kwa sababu katika uchunguzaji wa bidhaa kama ambavyo tumetembea katika taasisi za wenzetu na zaidi ile taasisi ya *TBS* pale Bara, tumekuta kwamba wana maabara za kila aina ili kupima viwango vya bidhaa tofauti. Sasa katika kufuatilia hili pia imeonekana kwamba zinahitajika fedha zisizopungua bilioni tisa kwa ajili ya kujenga maabara pamoja na kuweka vifaa vyake ili iweze kufanya kazi.

Hivyo basi, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba wawe na subira wakati shirika hili tunakazana nalo liweze kusimama wenyewe liweze kujitegemea, kwa sababu si kwamba bidhaa zinazoingizwa nchini hazipimwi viwango vyake. Lakini kama ambavyo tulivyokuwa tukifanya huko nyuma kwa mashirikiano makubwa kabisa na taasisi ya *TBS* pamoja na kuingiliana mikataba na wizara husika pale Bara, Mhe. Waziri wa Biashara wa Zanzibar lakini kwa mashirikiano na Mhe. Waziri wa Biashara wa Tanzania Bara tumeingiana mkataba kwamba wizara hizi kwa taasisi hizi mbili waendelee kushirikiana katika ukaguzi wa ubora wa bidhaa ambazo zitakuwa zinaingizwa nchini.

Hivyo, kazi inafanyika lakini si ndogo, kwa hiyo tutegemee baada ya muda si mrefu taasisi hii itakuwa inafanya kazi kama ambavyo tumetegemea au kama ambavyo imepangiwa katika mipango yake.

Mhe. Naibu Spika, vile vile limejitokeza suala zima la usindikaji wa mazao wa matunda. Tunafahamu kwamba suala la viwanda ni suala muhimu katika kuondoa tatizo la ajira nchini. Hivyo wizara ipo katika mpangilio wa kuandaa sera ambayo tunategemea itakamilika hivi karibuni. Sera hii ya viwanda ikishakamilika basi Wajumbe wa Baraza lako watapa taarifa. Pia tunatafakari umuhimu mzima wa suala la usindikaji wa mazao ya matunda.

Kwa hivyo, suala hili nalo wizara imejipanga pia kulifanyia kazi, na kwa hivyo tunaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili wafahamu hivyo, na kwamba muda ujao *in shaa Allah* viwanda hivi ambavyo ni *Cottage Industries* kwa ajili ya ku-*process* au kusindika matunda basi navyo vitaweza kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, michango haikuwa mingi nimalizie na kiwanda hichi cha Makonyo kule Pemba.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kiwanda hichi ni cha siku nyingi na tunafahamu hivyo, na kutokana na ufahamu huo basi wizara kwa kushirikiana na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (*TIRDO)* wamekuja kutufanyia utafiti kuhusu kiwanda hicho, na hatua karibu zitakamilika, na taarifa kamili itapatikana kupitia utaratibu ambao tumejiwekea wa kutoa taarifa katika Baraza lako Tukufu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa kuwa baada ya Baraza hili tunaingia kwenye uchaguzi. Nichukue fursa hii adhimu kushukuru sana mashirikiano tuliyoyapa kutoka kwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na tuombeane dua *In Shaa Allah* Mwenyezi Mungu atujaalie wale watakaoweza kurudi, turudi salama tukiwa na afya, Mwenyezi Mungu atujalie sote turudi *in shaa Allah* ili tuweze kuendeleza kazi hizi za kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kutoa shukurani za pekee kwa wananchi wangu wa Jimbo la Fuoni. Nimefanya kazi nao vizuri sana kwa ukaribu, na kwa mashirikiano yao makubwa yameniwezesha kufanya majukumu haya kwa ufanisi mkubwa sana. Kwa hiyo, kupitia chombo hichi niendee kuomba imani yao kwangu.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa niwatakie wote Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu lakini na wananchi wote kwa jumla Ramadhani njema.

Mhe. Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe waunge mkono hoja yetu hii, ili bajeti yetu iweze kupita yale maagizo ambayo wametupa ndani ya Baraza hili tuweze kwenda kuyafanyia kazi, na matarajio yake yaweze kuonekana.

Mimi naunga mkono asilimia mia moja hotuba yetu hii ya Bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** *Bismillahi Rahmani Rahiim*. Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwanza kabisa nachukua fursa hii kumshukuru *Allah* kutujaalia siku ya leo Ramadhani ya pili tunaendelea na kazi zetu za Baraza kama kawaida, tuko katika hali ya uzima na afya, *alhamdu lillahi*.

Vile vile ninakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa jinsi ulivyoongoza kikao chako vizuri hadi kufikia kuchangiwa na Wajumbe 14 hapo jana katika bajeti yetu hii.

Ninaomba kwa heshima kubwa niwashukuru wote ambao wamechangia katika bajeti yetu hii, na ninaomba niwataje mmoja mmoja kama walivyochangia.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla amechangia kwa niaba ya Mwenyekiti,
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Mohammedraza Hassanali
Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
Mhe. Mussa Ali Hassan
Mhe. Saleh Nassor Juma

Mhe. Hassan Hamad Omar
Mhe. Bikame Yussuf Hamad
Mhe. Abdalla Mohammed Ali
Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Jaku Hashim Ayoub
Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
Mhe. Panya Ali Abdalla, na
Mhe. Abdi Mosi Kombo.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla tumepokea hoja na maswali pamoja na mapendekezo ya Waheshimiwa waliotajwa hapo juu kuhusu bajeti hii, na naomba kufanya majumuisho pamoja na kutoa ufafanuzi wa hoja hizo kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, imetoka hoja moja kuhusu habari ya taarifa za bei za vyakula muhimu baina ya Pemba na Unguja kwa kweli linaleta ukakasi fulani suala la bei.

Ni kweli kuna tofauti hiyo ya bei ya vyakula baina ya Pemba na Unguja, na hii inasababishwa na usafirishaji bidhaa kutoka Unguja kwenda Pemba. Kwa hivyo jambo muhimu hapa ni kuwa Pemba tuwe na bandari ambayo itaweza kuchukua meli zenye *containers*, kwa hivyo ule usumbufu wa kuleta mzigo Unguja kwanza halafu kupeleka Pemba utaondoka na utasaidia sana kupunguza bei za vyakula.

Bei hizi zimeongezeka kutokana na usafiri kutoka Unguja kwenda Pemba. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya kila liwezekanalo ili tuweze kuwa na bandari Pemba, ambayo itaweza kuchukua mizigo mikubwa, bidhaa za mwani na karafuu pia zinasumbuliwa na mpango huu huu wa kuongezeka bei wakati wa usafarishaji.

Usumbufu wanapata wafanyabiashara katika soko la Tanzania Bara kweli bado upo, lakini nataka niseme kwamba umepungua kwa kiwango kikubwa, ndio maana ukaona kwamba bidhaa zinazotoka Bara zinaongezeka mwaka hadi mwaka.

Hata hivyo zipo zinaendelea kero hizo za biashara, lakini mazungumzo katika vikao vyetu vya Kero za Muungano zinaendelea na ninaamini siku hadi siku bidhaa hizo zitapata ufumbuzi wake.

Vile vile kulikuwa na suala la maji kwa nini maji ya Zanzibar hayauzwi Bara. Tatizo la kupeleka maji Tanzania Bara halipo isipokuwa wanaotaka kupeleka maji Tanzania Bara lazima waende wakafanye *registration* katika *TFDA*. *TFDA* ni Shirika la Vipodozi na Vyakula lilioko Tanzania Bara, wakienda waka-*register* mambo yatakuwa mazuri na njia nyepesi kwa sababu tayari kampuni nyingi za maji Zanzibar wameshaji-*register TBS*.

Kwa hivyo *TFDA* wakifika pale wakaji-*register* maji haya yatakuwa Tanzania Bara bila ya mzozo wowote. Na yeyote yule atakayekuwa tayari amefanya *registration* na *TFDA* afike wizarani tutamsaidia.

Kumetokea hoja ya Mahonda kuna wafanyakazi Mahonda wameachishwa kazi Mhe. Mwakilishi anasema wananyanyaswa, hawanyanyaswi ila wameachishwa kazi kwa mujibu wa sheria na wanapeleka malalamiko yao mahkamani.

Mimi ningeomba malalamiko yale wayaondoe mahkamani. Mimi nimeshakwenda kiwandani nishaongea na mmiliki wa kiwanda na wametutaka tufanye mambo haya nje ya mahkama.

Kwa hivyo mimi kabisa nitashukuru sana kama nitashirikiana naye Mhe. Mshimba kwa suala hili nimeshaongea na waziri mwenzangu wa Utumishi wa Umma ili tukae pamoja, kwa hivyo nitafurahi sana kama nitampata na Mhe. Mshimba tuwe pamoja katika suala hili, ili wale wananchi wapate haki yao bila ya kupata usumbufu zaidi. Kiwanda kiko tayari kufanya mazungumzo na kipo tayari kulipa baada ya mazungumzo hayo.

Mhe. Naibu Spika, suala la uchanganyaji karafuu na makonyo ni suala muhimu sana kulizingatia wananchi wote na viongozi sote. Tumo katika hatua ya mwisho ya mchakato wa kupata *brand* ya karafuu, haiwezekani kwenda kupeleka karafuu ambazo zina takataka kibao, hili suala la *brand* mwisho litakuwa linauliwa na tamaa ya watu wachache. Kwa hivyo bado elimu hii nataka tutoe sote viongozi na wananchi wote walielewe kwamba kuongeza taka taka za makonyo ni suala baya sana ambalo linaathiri au litaathiri uchumi wa Zanzibar.

Suala la kuongeza bei ya karafuu naomba Wajumbe na wananchi wote mtambue kwamba dunia nzima; si India, si Indonesia, si Madagascar, si Comoros, hakuna hata nchi moja mkulima wa karafuu anapata asilimia 80 ya bei ya kuuzia, hakuna, na mimi niko tayari kum-*challenge* mtu yeyote.

Comoro, Madagascar wanalipwa dola 2 kwa kilo yaani shilingi 4000 kwa kilo, sisi tunalipa shilingi 14000 halafu mtu anasema tuongeze shilingi 5000, tukishaongeza shilingi 5000 tutawezaje kufungua Mfuko wa Karafuu, tutawezaje kuwahudumia wakulima wa karafuu, tutawezaje kutoa miche ya karafuu bure, haitowezekana. Lakini mimi na-*challenge* kwamba dunia nzima hakuna hata nchi moja ambayo ina mkarafuu mkulima anapata asilimia 80, hamna! Wakulima wote dunia nzima wanapata asilimia haizidi kutoka 20 mpaka 25 ya bei ya karafuu duniani.

Nawaomba wananchi waone namna gani Serikali yao inavyowahurumia na inavyotaka kuona kwamba karafuu zinarudishwa katika hadhi yake. Serikali

imepania kuona bei ya asilimia 80 nzuri sana kwa kuwapa wakulima wetu. Kwa hivyo mimi ningeomba tuamini kwamba Serikali imefanya kazi kubwa sana na uamuzi mkubwa sana wa kisera wa kuona kwamba inatoa asilimia 80.

Jengo linalotumiwa na JKU bado hatujalipata. Wizara yangu na wizara husika ya Vikosi tumo katika mazungumzo ambayo tunatarajia kwenda katika tija katika siku zijazo.

Kuhusu Taasisi ya *ZBS*, ninafurahi kwamba Naibu Waziri ameeleza kwa urefu kabisa naona itakuwa haina tatizo lolote.

Suala la Kiwanda cha Makonyo kilioko Wawi malalamiko haya ya moshi yamekuja hapa mwanzo na Mwakilishi wa Wawi alilisema kwa uchungu suala hili na sisi tukapeleka kampuni ya *TIRDO* kwenda kufanya utafiti.

Kampuni ya *TIRDO* imetoa suluhisho la suala hilo, bomba la moshi liongezwe na limeongezwa na kifaa maalum kitafungwa katika bomba hili ili moshi huo kuweza kuondoa nguvu zake za kwenda kuathiri wananchi. Kwa hivyo Serikali inachukua hatua na ninaamini kwamba wananchi wa Jimbo la Wawi hawatoathirika tena na moshi unaotoka katika kiwanda hicho.

Duniani sasa hivi suala la moshi katika viwanda si tatizo tena ni masuala ya kuweka vifaa vya kuweza kuondoa sumu katika moshi huo.

Suala la kuwasaidia wazalishaji wadogo wadogo wa Gulioni huu ni ushauri mzuri tumeupokea na tutaufanyia kazi, kwa kweli tutafurahi sana kupata maarifa kama haya. Mtu anapokuja akatoa uchambuzi wa kukosoa tu bila ya kutoa ushauri huwa anatupa tabu, lakini anayekuja akakosoa halafu akatoa ushauri sisi tunafurahi sana na ushauri huu ni mzuri tunauchukua.

Kuna suala hapa la Mhe. Raza ambalo amenambia nimuangalie Mwenyezi Mungu na mwezi huu. Niseme ukweli kuhusu suala hili na ninaamini kwamba suala lake ni muhimu na lina mantiki kubwa sana. Bei za bidhaa zote Tanzania zitapanda tukitaka tusitake si chakula tu.

Mafuta yameshuka bei duniani lakini kwa bahati mbaya sisi Zanzibar hatujui kama mafuta yameshuka bei duniani bei iko pale pale. Hii inatokana bei ya dola kuwa imepanda juu sana. Mimi nasema kwamba suala hili ni muhimu sana kuliangalia.

Sisi kama Serikali ya Zanzibar, kwa sababu sisi tatizo kubwa au changamoto kubwa ni kuwa na *fiscal policy* moja baina ya Tanzania Bara na Zanzibar hili ni tatizo kubwa sana. Zanzibar hata tujitutumue vipi uchumi wetu hauwezi kuwa na

makali yoyote ikiwa bado *fiscal policy* ya Tanzania Bara na Zanzibar iko moja, haiwezekani, na kwa mtindo huu Zanzibar hatuna njia ya kujitutumua hata siku moja. Hata uchumi wa Zanzibar ukapanda ikiwa uchumi wa Bara uko chini na sisi tutakuwa uchumi uko chini tu basi, sisi ni uchumi wa visiwa na wenzetu ni uchumi wa bara, ni mambo tofauti kabisa.

Tuangalieni Hongkong, tuangalieni China, tuangalie Macau. Hongkong ni China na China imeweza kubagua, Hongkong wanatumia Hongkong *dollars* na China wanatumia RMB. Sasa kwa nini Machina baada ya kwishakuchukua Hongkong na Macau yao wasiweke bei moja, wasiweke *currency* moja wakatumia RMB kote. Lakini waliweka mkakati ule wala tofauti hakuna kubwa sana. Dola moja ni RMB 6.2 na dola moja ni Hongkong dola 7.4.

Kwa hivyo tofauti ndogo sana, lakini tofauti hiyo hiyo Serikali ya China haikuchanganya sera za kiuchumi za Hongkong na za China; wameziweka mbali mbali. Kwa hivyo hakuna sababu yoyote ya kuchanganya *fiscal policy* ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kama hatukubagua mambo mawili haya, Zanzibar hata uchumi ukakua vipi utarudi nyuma kwa sababu *fiscal policy* ni moja na sarafu ni moja.

Kwa hivyo hapo ni changamoto ambayo kwamba lazima Zanzibar tuangalie namna gani tutaweza kulitatua katika kero za Muungano. Lakini ni dhahiri kwamba sarafu ya Tanzania imeanguka kutokana na ukosefu wa dola katika soko la sarafu.

Ni kweli dola imeongezeka thamani duniani kwa asilimia kumi lakini Tanzania tumeathirika kwa asilimia 30 mpaka 35. Kwa sababu dola imepanda kutoka 1650 mpaka imefika dola 2350, hii ni hatari haijawahi kutokezea.

Kwa hivyo Mhe. Raza ninaamini kwamba taratibu ya kwenda kuonana na Balozi wa Marekani si mbaya, ni nzuri, lakini ningeomba Serikali yetu tuishauri, tuishirikishe, taratibu za kidiplomasia zifuatwe hapo ndio tuweze kwenda katika Ubalozi wa Marekani na balozi nyengine kwenda kueleza kwamba tatizo la *ESCROW* si tatizo la Zanzibar ni tatizo la Tanzania Bara.

Ni kweli kwamba fedha hizi za misaada zikikosekana kuingizwa katika soko la sarafu linaathiri kwa kiasi kikubwa sana upatikanaji wa dola. Kwa hivyo Mhe. Raza mimi ninakubaliana naye moja kwa moja kwamba Zanzibar wenzetu Bara wanatuteketeza. Tunapata adhabu tusiyostahiki, ukimkumbatia mwenye kinyesi na wewe utanuka vile vile! Kwa hivyo hii changamoto ya Zanzibar tukae pamoja tushirikiane. Kama hatujakaa pamoja sote wazanzibari tukali-*address* tatizo hili kama ni tatizo la Zanzibar hatuwezi kupata suluhisho, lazima wazanzibari wote wawe kitu kimoja ndio itapatikana suluhisho la suala hili, bila ya hilo itashindikana.

Namuomba Mhe. Raza tushirikiane kwa pamoja wazanzibari sote ili tatizo la kiuchumi baina ya Tanzania Bara na Zanzibar liweze kutatuliwa utatuzi ambao utaleta tija kwa Zanzibar na kwa Tanzania Bara.

Tukiendelea Waheshimiwa fidia ya wanaoanguka mikarafuu.

Mhe. Naibu Spika, tumeunda Mfuko wa Karafuu ambao kila mtu mwenye karafuu alioanzia miaka 18 kwenda mbele ataingia katika mfumo wa Bima na atapopata hasara yoyote ile Bima itamshughulikia itamlipia gharama zake za Bima. Lakini wale wote ambao wameanguka mikarafuu wakaathirika kabla ya tarehe hii ya kufanya mfuko huu, iko sheria ya wafanyakazi namba 15 ya mwaka 1989 ambayo imerekebishwa mwaka 2005 kwa kutumia sheria hii kila aliyeanguka mkarafuu na akaathirika atapatiwa matibabu yake na fidia yake kwa kupitia Wizara ya Fedha.

Sheria hii ipo ningeomba wale wote walioathirika na mikarafuu waende katika Wizara ya Uwezeshaji wakapeleke malalamiko yao na vielelezo vyao Wizara ya Uwezeshaji itapeleka Wizara ya Fedha na kwa mujibu wa sheria hii watalipwa fidia yao bila ya matatizo yoyote. Lakini sasa hivi uko mfuko na kila atakayeanguka Bima itamshughulikia.

Mhe. Naibu Spika, suala la *ZSTC* imeanza majaribio kuwasaidia wazalishaji wadogo wadogo kuzalisha mafuta ya makonyo.

Mhe. Mshimba alisema mashine tuwape, tushawapa mashine 9 washapewa wananchi kwa majaribio na wakifanikiwa tutaendelea kuwapa mashine zaidi ili waweze kutoa mafuta ya makonyo na mafuta ya mimea kuongeza uzalishaji.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu bei ya mwani. Bei ya mwani kweli ni tatizo. Tatizo la kwanza mwani tunaozalisha Zanzibar ni mwani wa aina ya *spinosum*, *spinosum* bei yake iko chini kwa bahati mbaya ndio mwani tunaotoa sisi Zanzibar. Tungetoa *cottonii*, *cottonii* ni mwani ukienda Indonesia wanatoa *cottonii* kwa wingi sana na *cottonii* ndio ina bei nzuri, *spinosum* bei yake ni ndogo ndio maana ukaona hapa Zanzibar leo tunapata bei ndogo kwa sababu ya mwani tunaoutoa. Tusiangalie karafuu na mwani kuwa sawa sawa, karafuu zipo katika Shirika la *ZSTC*, Shirika la *ZSTC* ni shirika la Serikali, kwa hivyo limejinyima kila hali na kumpa mkulima asilimia 80. Mwani unafanywa na sekta binafsi sisi tumekaa nao kwa kweli hawawezi kutoa ruzuku wao lazima wanunue mwani wauze wapate faida.

Kwa hivyo kwa bahati mbaya sana bei ya mwani iko chini kweli lakini si chini kwamba wanadhulumiwa hapana, ni bei *spinosum* duniani ni ndogo. Tumejaribu utafiti wa kupanda *cottonii* lakini kwa bahati mbaya *cottonii* haimei vizuri katika

visiwa vya Unguja na Pemba. Utafiti unaendelea kuona vipi tutabadilisha kutoka *spinosum* kuja kwenye *cottonii.*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu magari yanayoingia nchini kuna mengine mabovu sana. Ni kweli tumeliona hilo lakini *ZBS* limeshafanya mipango tayari katika kipindi kifupi kijacho magari yote kabla ya kuingia Zanzibar yatakaguliwa sehemu iliyonunuliwa kwa mfumo wa *PVoC* ili kupunguza tatizo la viwango.

Tutahakikisha kwamba magari yote yanayoingia nchini yana sifa za kuingia nchini, hatutokubali kuwa Zanzibar iwe ni jaa la kuleta magari mabovu.

Kuhusu vifaa chakavu katika kingo za barabara. Sheria Nam.14 ya Biashara mwaka 2013 imeshapitishwa katika Baraza lako Tukufu, itafanya kazi ili kuondoa mizigo ya bidhaa chakavu zilizo katika barabara. Wazo lako vile vile tutalichukua kwamba ipo haja ya kuweka maeneo maalum ya biashara za bidhaa chakavu.

Hata magari ipo haja ya kuweka soko moja tu, unaweka pahali pamoja pana njia maduka ya magari yote yanawekwa pahali pamoja. Vifaa chakavu vikae pahali pamoja, hiyo ni rai nzuri na tunaichukua na tutaifanyia kazi, ahsante sana Mhe. Mussa kwa kuyaona hayo.

Kote duniani iko hivyo; ukienda Hong Kong kuna sehemu maalum ya kununua vifaa chakavu na sehemu maalum ya kununua magari chakavu, ukienda Singapore ni hivyo hivyo hata Dubai ni hivyo hivyo. Kwa hivyo, Mhe. Mussa mimi ninakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu biashara ya dagaa na samaki. Ni kweli kwamba wananchi wanafanya biashara hii, Mhe. Mwakilishi kasema pale kwamba jamani hebu tufanyeni hii kazi ki-*scientific* kabisa. Ni kweli serikali imeliona hili na ndio maana mwenyewe Rais akatoa agizo kufanyika utafiti wa kina kuhusu suala zima la biashara ya dagaa.

Sasa hivi hapo Maruhubi ni *gazetted area;* ni sehemu maalum ambayo isingestahiki kufanyiwa biashara ile au kazi ile. Maruhubi mazingira yameharibika sana, lakini serikali imestahamili licha ya mazingira kuharibika kutokana na idadi ya wafanyabiashara wanaofanya kazi pale na maisha yao wanaendesha pale.

Kwa hivyo, serikali imo katika mipango ya kuona taratibu gani ichukuliwe ili kuweza kuwaondoa sehemu ile pale, lakini kuwapa sehemu nyengine ambayo wataweza kuzalisha bidhaa za dagaa; kulikausha kwa njia ya ki-*scientific*, ku-*pack* kwa njia ya ki-*scientific* na ili waweze kupata tija zaidi.

Kwa hivyo, suala hili Mhe. Rais mwenyewe ameunda Kamati; Wizara yangu ( Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko)na Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunashirikiana, na katika kipindi kifupi basi tatizo la bidhaa ya dagaa litaondoka na wananchi wetu wataondokana na matatizo haya. Vile vile na itaondosha suala la kuharibu mazingira katika sehemu ambayo wananchi wanafanya biashara ya dagaa.

Usarifu wa mwani Mhe. Bikame amelizungumza hili. Ni kweli, na hili vile vile tunashirikiana na *UNIDO*, *UNDP* kuona kwamba tunapata mashine na teknolojia ya kuweza kuusarifu mwani na kuweza kuutumia. Lakini Wazanzibari tujue kama mwani ni chakula, wenzetu Indonesia mwani wanazalisha mwingi, lakini mwingi nao wanaula, sisi hata kidogo hatuuli. Kwa hivyo, tutakuja na programu ya kufahamisha kwamba chakula gani kinatumika katika mwani, na ni moja katika chakula muhimu na kitaweza kusaidia sana katika lishe za wananchi.

Wabanjaji kokoto tumelisikia suala hilo, tunalichukua na tutalifanyia kazi ili kuwasaidia kina mama ambao wanabanja kokoto.

Soko la Jumapili. Ni kweli soko hili limewekwa kwa ajili ya kuwaweka wachimbaji na wafanyabiashara wadogo wadogo, hivyo soko hili wakiingia watu wote ni wajasiriamali wanauza bidhaa za kununua na kuuza, wanaozalisha wote ni wajasiriamali.

Mjasiriamali ni mfanyabiashara mdogo mdogo anayeweza ku-*risque* fedha yake kuitia katika biashara bila ya kujali hasara. Kwa hivyo, zote ni biashara zinaruhusiwa mwenye biashara yake ya kuuza afike katika soko la Jumapili auze. Hata akauza kitambaa, akauza nguo, suruali, shati, sabuni ya kukogea, anaruhusika. Dunia nzima soko la Jumapili hawakatazwi kwenda kuuza bidhaa zao. Watu wote waruhusiwe kwenda kuuza bidhaa zao bila ya ubaguzi wowote.

Mhe. Naibu Spika, Mfuko wa JK na AK ni kweli ipo lakini ukiangalia inatoa misaada midogo midogo, biashara kubwa kubwa hawawezi ndio maana ikabidi watu waende katika mikopo ya mabenki. Kwa mfano, hapo mbele hapo pana Kiwanda cha Sabuni, sabuni za *spicing*, sabuni hizo kiwanda hiki kinahitajia milioni 25 za kununua *raw materials* za kuweza kuzitia katika kiwanda chao. Mashine wanazo, kila kitu wanacho lakini wakienda katika mfuko wa AK na JK wanapata milioni mbili, milioni mbili haziwezi kuwasaidia kuweza kuendesha kiwanda chao. Kwa hivyo, bado wanahitajia mkopo wa milioni 25 ambao huu huwezi kuupata isipokuwa katika mabenki, na benki riba ni kubwa, na *process* ni refu inawawia vigumu kuweza kuendesha viwanda vyao.

Waheshimiwa naamini kwamba mengi mliotupa hapa ni ushauri, na ushauri wote tunauchukua tutaufanyia kazi kwa kina, kuona kwamba yote mliyotuchangia hapa yana umuhimu wake, na tunayachukua na tutayafanyia kazi, na *in shaa Allah* yatapekwa katika kipindi kifupi na tutapata matunda ya michango yenu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda kutoa hoja kwamba bajeti yangu ijadiliwe. Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Waziri hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa *quorum* yetu inaturuhusu, tuko Wajumbe 41.

Kwa hivyo sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka 2015/2016 wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda! (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, sasa kwa heshima zote naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yangu.

## KAMATI YA MATUMIZI

### FUNGU R01 – WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri hajaona, ushaona? Ni ukurasa wa 693, tayari, haya tunaendelea!

| | |
|---|---|
| Kifungu 04 Idara ya Biashara | Shs. 139,276,000 |
| **Jumla Kuu** | **Shs. 139,276,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

### FUNGU R01 – WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

### KIFUNGU P01 PROGRAMU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

| | |
|---|---|
| Kifungu S01 Uendeshaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda Masoko | Shs.1,562,863,000 |
| Kifungu S02 Mipango, Sera na Utafiti | Shs.442,464,000 |

| | |
|---|---|
| Kifungu S03 Ofisi Kuu Pemba | Shs. 355,170,000 |
| **Jumla ya Kifungu** | **Shs. 2,60,497,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KIFUNGU P02 PROGRAMU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI**

| | |
|---|---|
| Kifungu S01 Ukuzaji Viwanda | Shs.171,024,000 |
| Kifungu S02 Maendeleo ya Ujasiriamali | Shs.720,451,000 |
| **Jumla ya Kifungu** | **Shs. 891,475,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KIFUNGU P03 PROGRAMU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA**

Kifungu S01 Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji Shs.423,927,

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipokuwa nikichangia nilimuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi juu ya suala zima la matumizi ya *TBS* na *ZBS,* na hili hasa linakuja katika masuala ya kutafuta soko la kuweza kufanya biasha zake. Sasa wakati alipokuwa akifanya majumuisho Mhe. Waziri sikumsikia akilizungumzia suala hili, hivyo nilikuwa naomba ufafanuzi kidogo katika hili.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa suala umelielewa?

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Mwenyekiti, suala lake nalielewa na alilijibu Mhe. Naibu Waziri suala lake. Ni kwamba *Zanzibar Bureau of Standards* na *TBS* ni Tanzania nzima tume-*sign* mkataba baina ya *ZBS* na *TBS*…

**UTARATIBU**

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Lakini hatusikii kutokana na minong’ono ya watu kwa hiyo tunaomba…

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Subeit ondoka rudi pahala pako!

Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri anafanya majumuisho anaulizwa maswali anajibu, wengine wanazungumza, si utaratibu mzuri!

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Kweli Mhe. Mahmoud ameeleza suala hili na Mhe. Naibu Waziri wangu hapa amelijibu suala hilo, lakini kwa kweli tuna mashirikiano baina ya *TBS* na *ZBS*, tume-*sign* mkataba wa mashirikiano baina ya sisi na wao, kwa sababu wao wenzetu wana maabara tisa, sisi tutaanzisha maabara mbili tu, ndio hesabu za karibuni.

Kwa hivyo, ili *ZBS* ipate kulelewa tumetia mkataba na *TBS* ili kufanya kazi kwa pamoja katika masuala mengine mbali mbali, kama Tanzania. Kwa hivyo, suala la viwango kwa Zanzibar tunashirikiana kweli na *TBS* na wanatupa mashirikiano makubwa sana. Kwa hivyo, viwango vya Zanzibar na vya Bara vitakuwa vinatumia *standard* moja, na hiyo basi itasaidia sana bidhaa za Zanzibar kwenda Bara kwa njia rahisi kabisa bila matatizo yoyote.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri inaonekana hiyo ndiyo faida ya Muungano. Ahsante tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu kuhusu hoja ya mlango wa duka la vioo bado hajajenga uwezo aliotoa Mhe. Naibu Waziri.

Pana *tender* zimetangazwa kama eneo linataka kujengwa nyumba ya ghorofa, eneo lile nafikiri silo, kuanzia barabara kuendelea mbele kule, na kama lile duka alilokodishwa ule muda wake yule jamaa, muda wake ushakwisha na sifikirii kama atakodishwa tena kwa muda huu hadi kumaliza *tender*.

Sasa wajenge hoja zile barua zilizokuwepo za *tender* iliyokuwepo wazifungue ili kama panajengwa ghorofa lile duka limefulilizwa kujengwa, duka haliridhishi muda huu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante wakati nilipokuwa nikijibu suala alilouliza Mhe. Jaku tumesema kwamba *tender* hizo ziko katika utaratibu wa kufunguliwa, kwa sababu mkataba ule unaisha mwisho wa mwezi huu wa sita, na mambo yote yakienda sawa katika kipindi cha mwezi mmoja *tender* hizo atasikia zimefunguliwa kuanzia sasa.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, si vibaya mwezi huu mtukufu wa Ramadhani tukajulishana kama hadithi moja ndogo ya Mtume Muhammad (S.A.W) inayosema; "*Aayatul-munafiq thalatha"*.

Maana yake alama za mnafiki ni tatu; *idhaa hadatha kadhaba*, anapozungumza huwa anazungumza uongo, *waidha waada akhlafaa,* na anapotoa ahadi hatimizi, la tatu; *waidhantumina khaana,* na anapoaminiwa hufanya khiyana!

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku kaa. Mheshimiwa Naibu Waziri!

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Mwenyekiti, kauli anazozitoa Mhe. Jaku humu ndani haziridhishi hata kidogo, hatukutai kuchukua *quotation* za kidini, lakini sidhani kama ni sahihi kuita sisi ni wanafiki humu ndani, naomba afute kauli yake.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku tunataka tufuate utaratibu wa Baraza, kuna Kanuni zinatuongoza, lugha tunayotumia tutumie lugha ya ndani ya Baraza, maneno ya kupopoa popoa hatuyataki! Waziri kajibu hivi, kwamba *tender* inamalizika mwezi wa sita ya huyo aliyekodishwa, *tender* zitafunguliwa wakati wowote katika mwezi huu wa sita ama mwanzoni mwa mwezi wa saba. Sasa hoja yako kama hujaridhika twambie kitu gani?

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, mimi sibahatishi huu ni mwezi mtukufu wa Ramadhani nauheshimu, nimefunga hata sauti yangu haiwi kali kama kawaida yangu kuheshimu mwezi huu.

Mhe. Mwenyekiti, sizungumzi kwa kubahatisha haya maneno si yangu, wenye gazeti, na haya maneno ya Mtume Muhammad (S.A.W) sote karibu ni Waislamu humu, si maneno yangu, ni hadithi, kama anaipinga ndugu yangu Mama Thuwaybah, ni hadithi hii siwezi kupinga na ushahidi upo aniulize nithibitishe. Aniulize tu kwa heshima kabisa, nathibitisha haya ninayoyazungumza niko tayari kumthibitishia, *tender* imeandikwa hii hapa ngoja…

**Mhe. Mwenyekiti:** Hoja yako nini?

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Hoja muda mrefu wameandika hapa, maombi yanatakiwa kufungwa vizuri na kuwasilishwa kwa anuani iliyopo chini kabla ya saa nane mchana tarehe 30 Machi 2015.

Leo mwezi gani Mhe. Mwenyekiti, hebu nisaidie Mhe. Mwenyekiti kwa heshima kabisa, tarehe 30 Machi mpaka tunaleta humu mjadala wananchi hiki chombo ni kwa niaba ya wananchi.

Kwa heshima kabisa Mwenyekiti huu mwezi mtukufu wa Ramadhani kufika pahali tukatesana kama hivi tunafanya haki kweli Mheshimiwa? Muda mrefu walitoa tunaangalia wiki mbili hakuna kufungua bahasha, haichukui muda mrefu, bahasha

zenyewe tano au sita kufungua tu zitachukua muda wa miezi miwili au mitatu, pana jambo hapa. Huu ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani tuambizane ukweli. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe Mwenyekiti, naomba na mimi ni-*quote* Kanuni za Baraza, kwa sababu tunafahamu fika kwamba Mhe. Jaku ni *interested partner* katika hili. Kwa Kanuni ya 59(9) naomba niinukuu inavyosema. Inasema kwamba,

> "Mjumbe hatazungumzia jambo lolote ambalo yeye mwenyewe ana maslahi nalo binafsi isipokuwa baada ya kutaja namna halisi ya kiwango cha maslahi hayo".

Tunaomba a-*declare interest* hapa lakini jibu ni hilo. Baada ya mkataba kumalizika kama nilivyosema narudia, tutafungua *tender* hizo katika kipindi cha mwezi mmoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim kwanza jibu umelikubali au umelikataa. Wanasema mwezi wa sita unamalizika wanasoma *tender* mpya, watafungua hizo *tender* zote zilizopelekwa waliyoomba atakayebahatika atapata, aliyekosa ataomba kwengine. Hilo umeridhika kwanza halafu fungua kanuni.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti sijasikia wanafungua lini?

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Naibu Waziri anasema hivi, mwezi wa sita kodi ya *tender* ya duka la vioo inamalizika. Sasa baadae watasoma hiyo *tender* iliyoombwa kwa anayetaka kukodi. Kwa hiyo, kama umekodi wewe, kuna mtu mwengine atakayebahatika kupata atapata aliyekosa, atatafuta kwengine.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, yeye alikuwa ataje tarehe tu, nikishakuisikia nitahoji tarehe gani, maana yake anasema mwezi wa sita na mwezi wa sita unamalizika ni tarehe ngapi, mwezi wa saba au mwisho wa mwezi huu? Kwa sababu muda wake umeshakwisha yule mpangaji na serikali inahitaji mapato. Mimi ni mjumbe wa kamati wala asije akafikiria kama nina *interest* ya suala hili, mimi najua sana taratibu kama kuna mkono wangu mle ndani hizo *tender*...

**Mhe. Mwenyekiti:** Wameshaelewa subiri majibu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ataje tareje lini zitafunguliwa, haya mazowea ya siku zote ya serikali majibu nishayasikia mimi, ataje ni tarehe ngapi.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Mwenyekiti, tarehe hatutaji, hatujui tarehe gani, lakini yeye Mheshimiwa ni *interested partner*, huwezi kumruhusu akaeleza suala hili, yeye ame-*tender* kwangu kaja mara tano kuomba, barua yake ya ombi ninayo ofisini. Barua yake ya ombi ninaipeleka kwa Mhe. Waziri wa Fedha. Yeye ni *interested partner* asitusumbue. Hawezi kuzungumza kwa munkari, kuwa na kanuni tukaziweka katika madroo haiwezekani, kanuni itumike Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub tunaendelea.

**KIFUNGU P03 PROGRAMU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA**

Kifungu S01 Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji

*(Hapa Mhe. Jaku Hashim alisimama)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Nakwambia kaa kitako, mimi ndiye ninayeongoza kiti nakuomba sana uniwekee heshima, mimi ndiye ninayeongoza.

| | |
|---|---|
| Kifungu S01 Ukuzaji wa Masoko na Usafirishaji | Shs. 423,927,000 |
| Kifungu S02 Ushindani wa kibiashara na kumlinda mtumiaji | Shs.142,360,000 |
| Kifungu S03 Urahisishaji wa Biashara na Ukuzaji Biashara za Ndani | Shs. 690,041,000 |
| **Jumla ya Kifungu:** | **Shs. 1,256,328,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KIFUNGU P04 PROGRAMU YA VIWANGO NA THAMANI YA UBORA**

| | |
|---|---|
| Kifungu S01 Viwango na Udhibiti wa Ubora | Shs. 2,100,000,000 |
| **Jumla ya Kifungu:** | **Shs. 2,100,000,000** |
| **JUMLA KUU:** | **Shs. 6,608,300,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha za wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Naibu Spika, naafiki.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale waliokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka 2015/2016 wanyooshe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 - Wizara ya Fedha

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu muumba mbingu na ardhi kwa kutujaalia neema ya uhai na afya njema pamoja na kuendelea kuwepo kwa amani, utulivu na usalama wa nchi yetu uliotuwezesha kukutana hii leo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena napenda kumshukuru sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake uliojaa hekima na busara kwa nchi yetu. Nawashukuru pia, wasaidizi wake wakuu, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais kwa msaada na miongozo yao kwangu binafsi na kwa watendaji wa wizara yangu kwa madhumuni ya kuimarisha ufanisi wa kiutendaji wa majukumu ya wizara yangu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla natoa shukurani zangu kwako wewe, kwa kutuongoza hapa Barazani hadi leo hii tunakaribia kuhitimisha kikao hiki muhimu cha Baraza kilichopitia, kushauri na kuidhinisha mapendekezo ya bajeti za wizara mbali mbali za Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kushirikiana katika kikao hiki ambacho kinakamilisha mtiririko wa vikao tulivyovianza tokea mwishoni mwa mwaka 2010. Aidha,

namuomba Mwenyezi Mungu awalaze pema peponi wale wote ambao tulianza nao katika Baraza lako tukufu na kutokana na rehema zake hatukuweza kumaliza nao.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwapa pole wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla walioathirika na mvua zilizonyesha katika kipindi kifupi kilichopita cha masika. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa watendaji wote wa Wizara ya Fedha, wanaoongozwa na Ndugu Khamis Mussa Omar, Katibu Mkuu-Wizara ya Fedha, Wakuu wa Idara na Taasisi pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara kwa michango na ushirikiano wao mwema wanaonipa katika kuendelea kutekeleza majukumu yangu katika kuendesha wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba nianze kwa kuwakumbusha Wajumbe wa Baraza lako tukufu, majukumu ya Wizara ya Fedha kwa ujumla. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo:

i. Kuandaa, kutoa miongozo na kusimamia bajeti ya serikali;
ii. Kusimamia uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma (ikiwemo ufuatiliaji wa mapato ya ndani na nje, kusimamia matumizi ya serikali pamoja na kutoa huduma za kiuhasibu serikalini);
iii. Kusimamia mali, mitaji ya serikali iliyowekezwa katika kampuni mbali mbali pamoja na mashirika ya umma;
iv. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera na sheria za sekta ya fedha;
v. Kusimamia kwa ukamilifu Deni la Taifa na; na
vi. Kusimamia sekta ya fedha nchini na maendeleo yake.

## A. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

### a. Mapato ya Wizara kwa mwaka 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwasilisha utekelezaji wa majukumu ya wizara yangu kwa kutoa muhtasari wa mapato yasiyokuwa ya kodi yaliyokusanywa na wizara kwa mwaka wa fedha 2014/15. Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi 9,207.50 milioni kutoka katika vianzio tofauti visivyokua vya kodi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Mei 2015, wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi 8,799.89 milioni na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Mapato haya ni sawa na asilimia 96 ya makadirio. Kwa kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji, mapato yasiyokua ya kodi yaliyokusanywa na wizara yameonekana kukua mwaka hadi mwaka na kufikia Shilingi 8,799.89 milioni kutoka Shilingi 5,743.94 milioni zilizokusanywa mwaka

2010. Ongezeko hili linachangiwa na jitihada mbali mbali zinazochukuliwa na wizara zikiwemo; kuimarisha ufuatiliaji wa mapato yatokanayo na viza za wageni wanaongia nchini kwa kuweka mfumo wa ukusanyaji wa kupitia benki pamoja na Kufuatilia gawio la faida kutoka mashirika na makampuni ambayo serikali imewekeza.(Kiambatanisho namba I kinahusika).

**b. Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015**

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, wizara iliidhinishiwa matumizi ya Shilingi 101,587.00 milioni ikijumuisha Shilingi 31,786.67 milioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 69,800.00 kwa matumizi ya huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Mei 2015, wizara ilitumia jumla ya Shilingi 82,050.85 milioni sawa na asilimia 81 ya makadirio ya mwaka. Kati ya matumizi hayo, jumla ya Shilingi 23,800.48 milioni zilitumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha ulipaji wa mishahara ya wafanyakazi Shilingi 4,343.00 milioni, Shilingi 15,023.00 milioni zimetumika kama ni ruzuku kwa taasisi zilizopo chini ya wizara, Shilingi 4,434.55 milioni zimetumika kwa ajili ya kuendeshea shughuli mbali mbali za Wizara na Shilingi 58,250.37 milioni zilitumika kwa ajili ya huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali.

Aidha, wizara ilitumia jumla ya Shilingi 30,369.86 milioni kwa utekelezaji wa miradi na programu mbali mbali za maendeleo sawa na asilimia 73 ya makadirio ya Shilingi 41,500.00 milioni ya mwaka 2014/2015. Matumizi hayo yamejumuisha mchango wa Serikali wa Shilingi 21,869.86 milioni pamoja na Shilingi 8,500.00 milioni ikiwa ni mchango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka wa 2014/2015 wizara imekamilisha mradi wa Uimarishaji Utawala Bora awamu ya pili, mradi wa Kuimarisha Misaada Zanzibar pamoja na Ujenzi wa Meli ya Abiria ya Serikali. Viambatanisho namba II, III, IV na XI vinahusika.

**c. Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015**

**i. Kuandaa, kutoa miongozo na kusimamia bajeti ya Serikali**

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza jukumu hili, Wizara ya fedha inafanya tathmini ya makadirio ya rasilimali fedha na kuzigawanya rasilimali hizo kisekta, kutoa miongozo ya matayarisho ya Bajeti ya Serikali kwa kila mwaka pamoja na kusimamia malipo ya mishahara ya Wafanyakazi wa Serikali. Jukumu hili linasimamiwa na Idara ya Bajeti.

## IDARA YA BAJETI

Mhe. Naibu Spika, idara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015, iliendelea kutoa taaluma ya bajeti kwa jamii na hatimae kufanikisha utayarishaji wa bajeti ya Serikali kupitia mfumo wa programu (*PBB*). Kuandaa vitabu vya Bajeti ya mwaka 2015/16 kwa ajili ya mjadala wa Bajeti katika Baraza la Wawakilishi pamoja na kuendelea kufanya marekebisho ya mishahara ya watumishi serikalini. Aidha, idara imekamilisha utaratibu mzima wa marekebisho ya bajeti kutoka mfumo uliozoeleka wa vifungu kwenda katika mfumo mpya unaozingatia matokeo ya utekelezaji wa programu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, idara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 26,724.87 milioni, kati ya Fedha hizo Shilingi 8,500 milioni kwa ajili ya marekebisho ya mishahara serikalini, Shilingi 17,452.30 milioni kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Shilingi 772.57 milioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Idara. Hadi kufikia mwezi Mei 2015, idara imetumia jumla ya Shilingi 15,576.60 milioni sawa na asilimia 89 ya makadirio, ambapo Shilingi 15,023.00 milioni zimetolewa kwa ajili ya ruzuku za taasisi zilizo chini ya Idara na Shilingi 553.60 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida za Idara.

### ii. Kusimamia uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za Umma.

Mhe. Naibu Spika, Jukumu la kusimamia uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za Umma (ikiwemo ufuatiliaji wa mapato ya ndani na nje, kusimamia matumizi pamoja na kutoa huduma za kiuhasibu serikalini) liko chini ya Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali pamoja na Idara ya Fedha za Nje.

## IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, idara ilisimamia ukusanyaji wa mapato ya Shilingi 328,624.00 milioni kutoka katika vianzio vya ndani hadi kufikia Mei 2015. Mapato hayo ni sawa na asilimia 85 ya makadirio ya mwaka ambayo ni Shilingi 386,800.00 milioni.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka mitano (5) ya utekelezaji, Mapato ya ndani ya Serikali yameongezeka kwa Shilingi 156,934.00 milioni kutoka Shilingi 171,690.00 milioni zilizokusanywa mwaka fedha 2010/2011. Ongezeko hili ni matokeo yaliyotokana na usimamizi mzuri pamoja na kuimarika kwa misingi bora ya ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Mhe. Naibu Spika, kwa miaka hii mitano tumeshuhudia ukuaji wa mapato unaokwenda sambamba na ukuaji wa uchumi .Uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa hadi kufikia Mei, 2015 umefikia asilimia 16 na unatarajiwa kufikia asilimia 17 ifikapo Juni, 2015.Kiwango hiki bado ni kizuri ukilinganisha na Uwiano huo kwa Tanzania Bara ambao ni asilimia 14 na kwa nchi za kanda ya Afrika Mashariki ni wastani wa asilimia 13.5.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa matumizi ya serikali, idara imefanikiwa kusimamia matumizi ya Shilingi 454,064.64 milioni sawa na asilimia 64 ya makadirio ya Shilingi 707,800.00 milioni ya mwaka wa fedha 2014/2015. Sababu kubwa iliopelekea matumizi haya kuwa chini ya lengo ni kupungua kwa fedha za matumizi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita, matumizi ya serikali yanaongezeka mwaka hadi mwaka kwa madhumuni ya kukidhi mahitaji ya serikali yanayolenga kuimarisha huduma pamoja na kuleta maendeleo kwa wananchi. Katika kuhakikisha kuna usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma, idara inaendelea kuchapisha vitabu vya risiti vilivyowekwa alama maalum ya serikali ambayo haitaweza kunakiliwa na kutumiwa kinyume cha makusudio yake. Idara pia inaendelea kutoa taaluma za kitaalamu kwa wafanyakazi wa kada za uhasibu na wakaguzi. Aidha, idara inaendelea kuimarisha mtandao wa udhibiti wa matumizi (*IFMS*) kwa kubadilisha mfumo uliopo wa *epicor* 7.3.5 kwenda *epicor* 10. Mfumo huo mpya unatarajiwa kuunganishwa na mfumo wa mashine za risiti za elektroniki pamoja na mfumo wa bajeti unaotekelezwa kiprogramu (*PBB*). Matumizi ya mfumo huu yanatarajiwa kuanza mapema ifikapo Julai 2015.

Mhe. Naibu Spika, Mfumo huu pia utawezesha kufanya usuluhisho wa mapato yote yanayokusanywa na wizara sambamba na kuwezesha kutoa stakabadhi kwa kutumia mfumo huu. Idara pia inahakikisha inatumia vizuri fursa zinazopatika katika teknolojia ya habari na mawasiliano ili kuimarisha uwajibikaji katika fedha za Umma, sambamba na hili Idara imeshajipanga kufanya malipo yote ya wazabuni wa Serikali kwa kutumia mfumo wa **“***Tanzania Interbank Settlement System (TISS)”.*

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara iliidhinishiwa kutumia jumla ya TZS 3,720.55 milioni. Matumizi halisi mpaka kufikia mwezi wa Mei 2015 yalifikia jumla ya TZS 3,400.83 milioni sawa na asilimia 91 ya makadirio ya kazi za kawaida.Kiambatanisho namba V na IX kinahusika.

## IDARA YA FEDHA ZA NJE

Mhe. Naibu Spika, Jukumu la kuratibu na kusimamia upatikanaji wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar linasimamiwa na Idara ya Fedha za Nje.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ilitarajiwa kuratibu na kusimamia upatikanaji wa mapato kutoka nje ya TZS 306,000.00 milioni zikiwemo TZS 265,400.00 milioni kupitia programu na miradi mbali mbali ya maendeleo, TZS 40,000.00 milioni za misaada ya kibajeti (*GBS*) na TZS 600.00 milioni ikiwa ni msamaha wa Madeni (*MDRI*).

Idara imeweza kufatilia upatikanaji wa TZS 100,421.38 milioni sawa na asilimia 32 ya makadirio ya mwaka. Mapato hayo yanahusisha mikopo TZS 58,618.00 milioni na ruzuku za TZS 24,695.74 milioni, misaada ya kibajeti ya TZS 16,338.00 milioni pamoja na TZS 769.64 milioni zilizopokelewa kupitia misamaha ya madeni. Upungufu wa mapato umetokana na kutowasilishwa vizuri kwa fedha za misaada ya kibajeti pamoja na kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi mikubwa iliotarajiwa kuanza mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, Kwa kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita, Idara imeweza kufanikisha uanzishaji wa mfuko wa Afya ambao lengo lake ni kuendeleza huduma za afya wilayani. Idara inaendelea kuimarisha uhusiano na Washirika wa Maendeleo ambao kwa kiwango kikubwa wanachangia maendeleo ya Zanzibar. Miongoni mwa Washirika hao ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika; Benki ya Dunia; Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika; Umoja wa Ulaya; IFAD; OPEC na Taasisi za Umoja wa Mataifa; Serikali ya Marekani (USA); Sweden; Norway; Denmark; China; Nertherland; Spain, Saudi-Arabia pamoja na Japani.

Mhe. Naibu Spika, Changamoto kubwa inayoikabili Serikali ni kutokuwa na uhakika wa upatikanaji misaada kama ilivyokusudiwa. Ili kukabiliana na changamoto hii Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na kudhibiti mianya ya uvujaji na ukwepaji wa kodi.

Aidha, tathmini ya taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba mikopo nafuu imeongezeka na ruzuku zimeshuka. Hii inamaanisha kuwa Zanzibar kama nchi zinazoendelea inakuwa kiuchumi. Kiambatanisho V na XII kinahusika.

Mhe. Naibu Spika, Idara katika mwaka 2014/2015, iliidhinishiwa jumla ya TZS 283.44 milioni kwa kazi za kawaida. Matumizi halisi hadi kufikia mwezi wa Mei 2015 ni TZS 253.39 milioni sawa na asilimia 89 za makadirio ya mwaka.

**iii. Kusimamia Mali, mitaji ya Serikali iliyowekezwa katika kampuni mbali mbali pamoja na mashirika ya Umma**

Mhe. Naibu Spika, Jukumu la kusimamia mali, mitaji ya Serikali pamoja na kusimamia upatikanaji na uondoshwaji wa mali linasimamiwa na Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma.

**IDARA YA UHAKIKIMALI NA MITAJI YA UMMA**

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/15, Idara imesimamia upatikanaji wa TZS 3,920.00 milioni kama ni mapato yatokananyo na ukodishwaji na uwekezaji wa mali za Serikali. Mapato hayo sawa na asilimia 123 ya makadirio ya TZS 3,200.00 milioni kwa mwaka.

Mhe. Naibu Spika, Kwa kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita, Kiujumla Idara imefanikisha kutekeleza majukumu yafuatayo: kusimamia upatikanaji wa gawio la TZS 13,521.67milioni kutokana na mitaji iliyowekezwa katika makampuni na mashirika mbali mbali; kurejesha umiliki wa Serikali wa eneo lililokuwa likitumiwa na kampuni ya Zanzibar *Edible Oil* lililopo maeneo ya Amani, kurejesha umiliki wa kiwanda cha uzalishaji wa vifaranga vya kuku *ZAPOCO* kilichopo katika eneo la Maruhubi na mashamba yake pamoja na kiwanda cha *ZAFICO* Malindi.

Mhe. Naibu Spika, Idara kwa kushirikiana na mshauri elekezi imeweza kuzitambua mali za Serikali za Wizara tano kwa kuziwekea alama tambuzi *Codification* na kuziweka katika daftari la kumbukumbu *Asset Register*, jumla ya mali zenye thamani ya TZS 1,420,584.30 milioni zimetambuliwa. Kadhalika mali za Serikali zinaendelea kufanyiwa tathmini na ifikapo mwaka 2017/18 matarajio ni kwamba mali zote za Serikali zitakua zimetambulika. Idara imehakikisha kwamba manunuzi yote ya Wizara na Taasisi za Serikali yanasimamiwa na Bodi za Zabuni zilizoanzishwa kwa mujibu wa sheria ya manunuzi no.9 ya 2005.

Aidha, Idara imesimamia ufufuaji wa Kiwanda cha Sukari na katika kipindi cha majaribio kiwanda kimeweza kuzalisha tani 200 za sukari. Kiwanda hicho kinaendelea kufanya mabadiliko makubwa kwa kuweka mashine mpya na baada ya kukamilisha kitakuwa na uwezo wa kuzalisha hadi tani 80 kwa siku na kutoa ajira kwa wafanyakazi wasiopungua mia saba (700). Idara pia imesimamia ujenzi wa Ofisi nne (4) za Serikali, zikiwemo; Ofisi ya Makamo wa pili wa Rais; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ofisi ya Katiba na Sheria pamoja na kuendelea na usimamizi wa jengo la Chuo cha Uandishi wa habari-Kilimani.

Mhe. Naibu Spika, Katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2014/2015, Idara iliidhinishiwa kutumia jumla ya TZS 415.00 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Mei 2015, jumla ya TZS 367.01 milioni zilitumika ikiwa ni sawa na asilimia 88 ya makadirio.

**iv. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera na sheria za sekta ya Fedha**

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Fedha ina jukumu la kuibua na kuzipitia Sera, Sheria na kanuni mbali mbali za Fedha kwa madhumuni ya kuendeleza mageuzi ya msingi ya sekta ya fedha. Jukumu hili linatekelezwa kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka 2010 hadi 2015, Sheria mbili (2) zimeshafanyiwa mapitio na zinaendelea na taratibu za kuzithibitisha katika ngazi tofauti za uongozi. Idara imekamilisha Sheria na kanuni ya Sheria ya Utakasaji wa Fedha haramu *Ant-Money laundering regulation*. Idara imekamilisha sera ya huduma ndogo ndogo za fedha *Microfinance Policy* nayo pia inaendelea na taratibu za kuthibitishwa katika ngazi tofauti za uongozi. Aidha, Idara inaendelea kusimamia vikao vya Bodi ya Rufaa ya Kodi kwa ajili ya kutatua migogoro ya walipa kodi, hadi kufikia Mei 2015 jumla ya kesi tano (5) zimesikilizwa ambapo kesi mbili (2) zimeshatolewa maamuzi.

Mhe. Naibu Spika, Katika kutumia fursa za kiuchumi zinazoweza kupatikana katika mitangamano ya kikanda, Idara inaendelea kushiriki katika vikao tofauti vya kikanda vinavyohusu masuala ya fedha, vikiwemo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki *EAC* pamoja na Mikutano ya utatu Tripatite-*SADC*, *COMESA na EAC* kwa ajili ya kulinda maslahi ya nchi. Kwa mwaka 2014/15, Idara iliidhinishiwa jumla ya TZS 241.84 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Mei 2015, Idara imetumia jumla ya TZS 201.90 milioni sawa na asilimia 83 ya makadirio.

**IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI**

Mhe. Naibu Spika, Idara hii ndio yenye jukumu la kuweka mazingira bora ya kazi na kusimamia huduma za *TEHAMA*. Kwa mwaka wa fedha 2014/15, Idara imeendelea na kazi zake za kuwajengea uwezo wafanyakazi 17 wa Wizara kwa kuwapeleka katika mafunzo ya muda mrefu na jumla ya wafanyakazi 12 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi; kuwapatia likizo watendaji 90; kuandaa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi 50 kwa lengo la kuelewa vizuri sheria ya

Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011; na Idara imeendelea kuimarisha ofisi na kuwapatia vitendea kazi vinavyokwenda na wakati wafanyakazi wake.

Mhe. Naibu Spika, Kwa kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji, Wizara imeweza kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma kwa masomo ya muda mrefu ambapo wafanyakazi 55 katika ngazi ya Shahada ya Pili, wafanyakazi 65 katika ngazi ya Stashahada ya Juu, 74 katika ngazi ya Shahada ya Kwanza na, wafanyakazi 19 katika ngazi ya Stashahada ya Kawaida.

Mhe. Naibu Spika, Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya TZS 3,406.66 milioni kwa utekelezaji wa majukumu yake. Hadi kufikia mwezi wa Mei 2015, Idara imetumia jumla ya TZS 3,103.17 milioni sawa na asilimia 91 ya makadirio ya mwaka.

**OFISI KUU - PEMBA**

Mhe. Naibu  Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/15,Ofisi kuu Pemba imeendelea kuimarisha mazingira bora ya kazi ; kuhakiki mali za Serikali pamoja na ukaguzi wa manunuzi katika Ofisi na Taasisi za Serikali zilizopo Pemba; kusimamia na kuimarisha shughuli za uhasibu Serikalini kwa upande wa Pemba; kuratibu na kusimamia malipo ya viinua mgongo na pencheni kwa wastaafu wanaopokelea pencheni zao Wizara ya Fedha kupitia Ofisi kuu Pemba; kuwapatia mafunzo na kuwaweka tayari watumiaji wapya wa mtandao wa *IFMS* kwa Wizara na Taasisi za Serikali; kuratibu majadiliano ya bajeti kwa vikundi vya jamii na taasisi zisizo za kiserikali Pemba; na kuratibu upatikanaji wa mafunzo ya bajeti ya programu (*PBB*) kwa maafisa wadhamini pamoja na watendaji mbali mbali kwa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Ofisi ya kuu Pemba iliidhinishiwa jumla ya TZS 1,146.12 milioni kwa kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia Mei 2015, Ofisi hii imetumia jumla ya TZS 897.57 milioni sawa na asilimia 78 ya makadirio ya mwaka kwa matumizi ya kazi za kawaida.

**v. Kusimamia Deni la Taifa**

Mhe. Naibu Spika, jukumu la kusimamia deni la Taifa linasimamiwa na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kupitia Mfuko Mkuu.

**MFUKO MKUU WA SERIKALI**

Mhe. Naibu Spika, Deni la Taifa lililoripotiwa mwishoni mwa mwezi wa Mei 2015, limeongezeka hadi kufikia TZS 324,200.00 milioni, sawa na ukuaji wa asilimia 8.3 ikilinganishwa na deni lililokuwepo mwezi wa Mei 2014 la TZS

299,400.00 milioni. Deni la Nje limefikia TZS 224,000.00 milioni ikilinganishwa na TZS 213,800.00 milioni lililoripotiwa mwezi wa Mei 2014. Asilimia 88 ya deni la nje yanadhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na asilimia 12 ya deni hilo yapo chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Deni la ndani hadi mwishoni mwa mwezi wa Mei 2015 liliongezeka na kufikia TZS 100,200.00 milioni ikiwa ni ongezeko la asilimia 21 ikilinganishwa na deni la TZS 82,600.00 milioni lililokuwepo mwezi wa Mei 2014. Ongezeko hili limetokana na deni lililochukuliwa katika soko la ndani kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbali mbali za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, Deni la ndani limeongezeka kutoka TZS 36,635.35 milioni kwa mwaka 2010 na kufikia TZS100,186.31 milioni katika mwaka 2015. Uwiano wa Deni la ndani kwa mapato ya ndani bado ni wa kuridhisha. Hadi mwezi Mei 2015 uwiano huo ulifikia 3:1; hii inamanisha mapato ya ndani yangeweza kulipa deni la ndani mara tatu zaidi. Kiambatanisho namba IX na X kinahusika.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, jumla ya TZS 69,800.00 milioni ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Hadi kufikia mwezi wa Mei 2015 jumla ya TZS 58,250.40 milioni zimetumika ikiwa sawa na asilimia 84 ya makadirio. Kati ya fedha hizo, TZS 9,789.90 zilitumika kwa kulipia pencheni kwa wastaafu wa wastani wa 11,530 kila mwezi, TZS 7,425.1 milioni zilitumika kwa kulipia viinua mgongo kwa wastaafu 885 wa Serikali, TZS 14,030.20 milioni zilitumika kwa kulipia riba na mitaji ya mikopo iliyochukuliwa na Serikali katika vipindi tofauti na TZS 27,005.20 zilitumika kwa matumizi maalum ya Serikali.

**vi. Kusimamia sekta ya huduma za fedha nchini na maendeleo yake**

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya fedha ndio yenye jukumu la kusimamia sekta ya huduma ya fedha nchini pamoja na kufuatilia maendeleo yake. Hadi kufikia Mei 2015 Sekta ya huduma ya fedha nchini inajumuisha benki kumi (10), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Shirika la Bima, taasisi na huduma ndogo ndogo za kifedha zikiwemo Z-PESA, TIGO-PESA,M-PESA, BRAC, PRIDE, YETU *microfinance.*

Mhe. Naibu Spika, Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika ukuaji wa Sekta hii ya huduma za fedha kwa kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa awamu hii ya saba. Sekta ya huduma za kifedha imechangia asilimia 4.1 ya pato la taifa kwa mwaka wa 2014 ukilinganisha na uchangiaji wa asilimia 3.4 ulioripotiwa mwaka 2010. Aidha, amana za benki zimeongezeka kutoka TZS 311,900.00 milioni katika mwaka 2010 hadi kufikia TZS 536,800.00 milioni katika mwaka 2015. Mikopo inayotolewa na benki mbali mbali kwa wananchi kwa ajili ya kuendeshea shughuli za kiuchumi imeongezeka kutoka TZS 100,400.00 milioni hadi kufikia jumla ya

TZS 205,800.00 milioni katika mwezi wa Mei 2015. Kiambatanisho namba XIV kinahusika.

Mhe. Naibu Spika, Wizara imeandaa mikakati maalum ili kuhakikisha ukuaji wa Sekta hii unakidhi mabadiliko ya uchumi nchini pamoja na yale ya kidunia. Miongoni mwa mikakati hiyo ni; Kufanya utafiti wa kitaifa kwa kutumia"*Knowledge, Attitude and Practice model* (*KAP*)" katika mwaka 2015/2016 ili kutambua ni sababu gani inayowapelekea wananchi kutotumia zaidi huduma zinazotolewa na taasisi za kifedha; kuandaa sera, sheria na kanuni ili kuimarisha mazingira yatakayoweza kuwashawishi wananchi wote wa vijijini na mijini kutumia huduma za kifedha; kuongeza wigo wa biashara kwa kufungua matawi ya Benki ya Watu wa Zanzibar; Wizara inatarajia pia kuanzisha akaunti za uwekezaji kupitia Benki ya Kiislamu pamoja na kuongeza huduma za bima kwa kufungua bima ya kiisalam.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa taarifa za utekelezaji wa taasisi za kifedha zilizochini ya Wizara.

**BENKI YA WATU WA ZANZIBAR**

Mhe. Naibu Spika, Jukumu kubwa la Benki ya Watu wa Zanzibar *PBZ* ni kupokea amana za wateja wake na kuwakopesha wanaohitaji pamoja na kuwapatia wateja huduma mbali mbali za kibenki. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, hadi kufikia Mei, 2015 Benki ilitekeleza yafuatayo: Kupokea amana za wateja zenye kiwango cha TZS 91,700.00 milioni ikiwa ni asilimia 120 ya lengo lililowekwa la TZS 76,400.00 milioni; Amana za wateja kwa ujumla sasa zimefikia TZS 366,500.00 milioni ikiwa na ongezeko la asilimia 33 ikilinganishwa na amana zilikuwepo kipindi cha Mei 2014; Kutoa mikopo ya TZS 88,371.00 milioni sawa na asilimia 130 ya lengo lililowekwa la TZS 68,107.00 milioni (Mikopo iliyotolewa kwa wateja mbali mbali hadi sasa imefikia TZS 229,700.00 milioni). Aidha, Benki imefanikiwa kuongeza rasilimali za Benki kwa TZS 99,100.00 milioni ikilinganishwa na lengo la TZS 66,320.00 milioni (Rasilimali za benki kwa sasa zimefikia TZS 420,430.00 milioni).

Mhe. Naibu Spika, Kwa kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita 2010 hadi 2015, Amana za wateja zimeongezeka kwa TZS 247,496 milioni kutoka TZS 119,004.00 milioni zilizokuwepo mwaka 2010. Kwa upande wa mikopo nayo imeongezeka kwa TZS 196,244.00 milioni kutoka TZS 33,446.00 milioni zilizoripotiwa mwaka 2010. Rasilimali za benki nazo zimeongezeka kwa TZS 278,369.00 milioni kutoka TZS 142,061 milioni zilizokuwepo katika mwaka 2010. (Kiambatanisho namba XII kinahusika).

Mhe. Naibu Spika, Mafanikio haya yamechangiwa na mikakati mbali mbali iliyowekwa ili kuhakikisha benki yetu inakwenda sambamba na mabadiliko ya kidunia. Miongoni mwa mikakati hiyo ni: Uanzishwaji wa Benki ya Kiislamu katika mwaka 2011, ambayo imesaidia kuongeza idadi ya watumiaji wa huduma za kibenki *(Financial Inclusion).* Huduma za Benki ya Kiislam zinakuwa kwa zaidi ya asilimia 100 kwa mwaka hadi kufikia Mei 2015, Benki ya Kiislam ya *PBZ* inawateja 50,500 ikilinganishwa na wateja wanaotumia 4,000 waliokuwepo mwishoni mwa mwaka 2011, amana za wateja wanaotumia huduma hii sasa imefikia TZS 86,894 milioni.

Kwa upande wa mikopo inayofuata misingi ya sha'riah za kiislamu nayo imefikia TZS 29,020 milioni ambapo wakopaji ni wafanyakazi wa Serikali, taasisi za Serikali na Mashirika binafsi; kuimarishwa kwa huduma za benki kwa kuanzisha huduma kupitia *ATM*, simu za mkononi, intaneti pamoja na kutanua matawi yake Zanzibar na Tanzania Bara kutoka matawi matatu (3) mwaka 2010 na kufikia matawi kumi (10) na vituo vinne (4) vya kutolea huduma katika mwaka 2015; Kuanzishwa kwa huduma ya kusafirisha fedha kupitia mtandao wa *WorldRemit* kwa Watanzania wanaoishi Ughaibuni; Kuanzishwa kwa mikopo ya nyumba ambayo hadi kufikia Mei 2015, jumla ya TZS 1,230.00 milioni zimetolewa. Wateja wa *PBZ* kwa sasa wanafursa ya kupata huduma hii kwa lengo la kupata makaazi bora; Kuanzisha mfumo wa haraka wa kulipa hundi *(Tanzania Automated Clearing House).* Mfumo huu utawawezesha wateja wa *PBZ* wanaoleta hundi za benki nyengine kupata fedha zao ndani ya siku moja badala ya muda uliokuwepo wa siku nne; Kuanzisha mikopo ya Elimu ya juu kupitia Benki ya Kiislamu, jumla ya TZS 60.00 milioni zimetumika kwa kazi hiyo pamoja na kuanzisha huduma za ukodishaji vifaa mbali mbali (Ijara).

## MFUKO WA HIFADHI YA JAMII (*ZSSF*)

Mhe. Naibu Spika, Lengo la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni kutoa hifadhi kwa wanachama wake pale wanapopatwa na majanga kama maradhi, ulemavu, kifo au uzee. Majanga ambayo husitisha au kupunguza kipato cha mwanachama. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mfuko husajili wanachama waajiri na waajiriwa, hupokea michango, huweka kumbukumbu za wanachama, huwekeza ziada ya fedha zinazokusanywa pamoja na kulipa mafao kwa wanachama wake pale muda unapofikia kwa mujibu wa Sheria Namba 2 ya Mfuko.

Mhe. Naibu Spika, Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita idadi ya wanachama waajiri imeongezeka na kufikia 1,572 ikilinganishwa idadi ya wanachama 926 waliokuwepo mwaka 2010. Idadi ya wanachama waajiriwa nayo imeongozeka hadi kufikia 74,890 kwa mwaka 2015 ikilinganishwa na idadi ya wanachama waajiriwa 61,396 iliyokuwepo katika mwaka 2010. Michango ya wanachama pia

imeongezeka kutoka TZS 14,770.00 milioni iliyokusanywa mwaka 2010 na kufikia TZS 28,860.00 zilizokusanywa katika mwaka 2015.

Mhe.Naibu Spika, Mfuko umeweza kumaliza ujenzi wa Kiwanja cha kufurahishia watoto cha UHURU-Kariakoo, Mfuko uko katika hatua za mwisho kumalizia ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto cha UMOJA-Tibirinzi Pemba pamoja na Mnara wa Mapinduzi ulioko Michenzani.

**SHIRIKA LA BIMA - ZANZIBAR**

Mhe. Naibu Spika, Kwa kipindi cha mwaka 2014/2015, Shirika la Bima la Zanzibar, lilijipangia kutekeleza malengo mbali mbali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Utekelezaji halisi wa Shirika kwa mwaka 2014/2015 ni kama ufutavyo: Kwa upande wa mapato lengo la Shirika ni kukusanya jumla ya TZS. 15,524.00 milioni kutokana na vianzio mbali mbali vya mapato hadi kufikia Mei 2015 Shirika liliweza kukusanya TZS. 16,527.00 milioni ikiwa na ongezeko la asilimia 6 ya makadirio.

Mhe. Naibu Spika, Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, mapato ya Shirika yameongezeka kutoka TZS 8,141.74 milioni katika mwaka 2010 na kufikia TZS 17,604.48 milioni katika mwaka 2015. Wateja wanaotumia huduma za Shirika wameongezeka na kufikia 65,290 ikilinganishwa na wateja 64,574 waliokuwepo mwaka 2010. Sababu kubwa iliyopelekea kukua kwa mapato, ikiwemo ile ya kupanga viwango vipya vya ada.

Aidha, amana za Shirika zimekua kwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na amana za Shirika zilizokuwepo mwaka 2010. Mafanikio haya yanatokana na kuimarika kwa huduma za Shirika kwa kuongeza wigo katika eneo la Mtwara na kuanza kutoa huduma katika jengo lake jipya lilioko Mtaa wa Mpirani-Zanzibar kitu ambacho kimewavutia wateja wengi pamoja na ushirikishwaji wa wadau mbali mbali wa Bima.

Mhe. Naibu Spika, Shirika limeongeza mbinu bora za kutoa huduma zake kiurahisi na kujitawanya katika mikoa sita kwa upande wa Tanzania Bara kwa lengo la kuzidisha mapato yake ya mwaka na kutafuta dalali mwenye utaalamu wa mgawanyo wa matawi ya huduma za Bima *(Afro-Asian Broker)* anaetambulikana kimataifa kwa kazi zake wa Mtawanyo wa Bima.

Mhe. Naibu Spika, Sasa naomba niwasilishe Utekelezaji wa taasisi nyengine zilizo chini ya Wizara ya Fedha ambazo zinatoa huduma mbali mbali kwa wananchi na Serikali kama ifuatavyo:

## BODI YA MAPATO ZANZIBAR (*ZRB*)

Mhe. Naibu Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) ina jukumu la kukusanya mapato ya ndani ya Serikali. Kwa mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Bodi ya Mapato ilikadiriwa kukusanya jumla ya TZS 181,300.00 milioni. Utekelezaji halisi katika kipindi cha Julai-Mei 2015, *ZRB* imeweza kukusanya jumla ya TZS 160,829.92 milioni sawa na asilimia 89 ya makadirio ya mwaka. Makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 8.8 ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hiki cha mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo jumla ya TZS 146,597.71 milioni zilikusanywa.

Mhe. Naibu Spika, Katika kipindi cha miaka mitano kutoka 2010 hadi 2015 kiwango cha makusanyo ya kodi zinazosimamiwa na *ZRB* kimeongezeka kutoka TZS92,364.00 milioni katika mwaka 2010/2011 hadi TZS 162,245.00 milioni mpaka mwezi Mei 2015. Ongezeko hili linachangiwa na kuimarika kwa misingi bora ya ukusanyaji ikiwemo; Kuimarishwa usimamizi katika ukusanyaji wa mapato kwa kufanya ziara za mara kwa mara katika vyanzo vya ukusanyaji; kutumia huduma za *TEHAMA* katika ukusanyaji; Kutoa elimu kwa walipa kodi kwa kupitia vyombo vya habari vilivyopo nchini; kuimarisha ushirikiano katika masuala ya ulipaji kodi kutoka kwa taasisi za Serikali na zile zisizo za kiserikali; Kufanya marekebisho ya sheria na kanuni mbali mbali zinazosimamiwa na Bodi ya Mapato; Kufanya ukaguzi wa kina katika hoteli zinazopokea na kulaza wageni; kuwafuatilia walipakodi wenye deni pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Serikali ili kudhibiti biashara za Magendo. (Kiambatanisho na VI kinahusika).

Mhe. Naibu Spika**,** Bodi ya Mapato imetumia jumla ya TZS 7,608.33 milioni sawa na asilimia 92 ya makadirio ya mwaka ya TZS 8,300.00 milioni kwa kutekeleza majukumu yake iliyopangiwa.

## MFUKO WA BARABARA

Mhe. Naibu Spika, Mfuko wa Barabara umeendelea na jukumu lake la kuweka utaratibu madhubuti wa kutunza fedha za matengenezo ya barabara, kutoa fedha hizo kwa ajili ya matengenezo ya barabara pamoja na kufuatilia na kukagua matumizi ya fedha hizo kwa dhamira ya kuwa na miundombinu endelevu. Aidha, Mfuko una majukumu ya kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kwa ufanisi na kwa lengo lililokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, Katika 2010 hadi 2015, Mfuko wa Barabara umefanikiwa kutoa fedha na kufuatilia matengenezo mbali mbali ya barabara kwa kuitumia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano yakiwemo matengenezo ya kawaida kwa barabara zote za lami kwa kuzifanyia usafi na kuziba mashimo, kufanya matengenezo ya

barabara kwa kiwango cha lami jumla ya kilomita 51, kufanya matengenzo ya barabara za kifusi jumla ya kilomita 87, imesimamia ujenzi wa madaraja tisa na makalavati 12, imeimarisha usalama wa watumiaji wa barabara kwa kuweka taa za kuongozea gari na waendao kwa miguu sehemu ya Mkunazini , Kwa Mchina Mwanzo na inaendelea na uwekaji wa taa hizo eneo la Malindi. Aidha, Mfuko umefanikiwa kuimarisha mazingira ya Wafanyakazi wake kwa kujenga Ofisi yake ya kisasa iliopo Maisara pamoja na bustani iliyopo mbele ya jengo.

Mhe. Naibu Spika**,** Kwa mwaka wa fedha wa 2014/15, Mfuko wa Barabara ulilenga kupokea makusanyo ya jumla ya TZS 7,108.37 milioni ambapo TZS 7,102.00 milioni zikiwa ni kwa makusanyo yatokanayo na *"Road Development Levy"* na TZS 6.37 millioni kutokana na ukodishaji wa jengo. Kati ya fedha hizo jumla ya Tsh 6,189.37 milioni zilitengwa kwa kazi za matengenezo ya barabara na TZS 919.00 milioni kwa kazi za Uendeshaji Mfuko. Hadi kufikia Mei 2015, jumla ya Tsh 6,800.00 milioni zilishakusanywa ambazo ni sawa na asilimia 95 ya makadirio ya mwaka. Matumizi yalifikia jumla ya TZS 4,133.00 milioni sawa na asilimia 58 ya makadirio ya mwaka. Kati ya matumizi hayo jumla ya Tsh 3,361.00 milioni zililipwa kwa kazi za barabara zikiwa ni asilimia 54 ya makadirio ya mwaka. TZS 772.00 milioni zilitumika kwa kazi za Uendeshaji Mfuko zikiwa ni asilimia 84 ya makadirio kwa kutekeleza majukumu mbali mbali yaliyopangwa.

## MAMLAKA YA UWEKEZAJI NA VITEGA UCHUMI-ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka kwa mujibu wa sheria ina jukumu la kushajiisha wawekezaji wa nje na ndani pamoja na kurahisisha mchakato wa uwekezaji. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Mamlaka iliweka mkazo kuendeleza Maeneo Huru ya Uchumi – Fumba kwa kutayarisha mpango wa matumizi ya ardhi na kuanza ujenzi wa miundombinu ya barabara. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Mamlaka imetekeleza yafuatayo: Imekamilisha mzunguko wa saba wa Utafiti wa Mwenendo wa Mitaji Binafsi *(Private Capital Flow).* Utafiti umebaini kuwa mitaji binafsi inayoekezwa inaongezeka hususan katika sekta ya Utalii (Hoteli, Mikahawa na michezo ya baharini). Pia utafiti huo umebaini ongezeko la asilimia 18 la ajira iliyosababishwa na ongezeko la mitaji hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka pia iliendelea na tafiti nyengine zikiwemo za kubaini fursa mpya za uwekezaji kwa kushirikiana na *"Commission for Science and Technology (COSTECH)";* Uidhinishwaji wa miradi 20 inayotarajiwa kuingiza jumla ya mitaji yenye thamani ya TZS 703,150.00 milioni sawa sawa na USD 343 milioni ambazo zinatarajiwa kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 681, kati ya ajira hizo, ajira 545 zitatolewa kwa wazalendo; Mamlaka imekamilisha utayarishaji wa njia kuu zenye urefu wa kilomita 10.2 maeneo huru-Fumba na kukamilika kwa michoro ya kiufundi ya majengo yatayohusiana na miradi mbali mbali katika eneo

hilo. Aidha, Mamlaka imekamilisha taratibu za kimataifa zitakazowezesha wawekezaji kupata hifadhi juu ya mitaji yao pamoja na haki za msingi za wawekezaji na wananchi kwa ujumla. Pia Mamlaka inaendelea na utayarishaji wa Kongamano la kimataifa ambalo linatarajiwa kufanyika Disemba 2015.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka mitano ya awamu ya saba, Mamlaka imefanikiwa kusajili miradi 187 yenye thamani ya TZS 38,560.50 milion sawa sawa na USD 1,881.00 milioni ambayo inakadiriwa kuzalisha ajira zipatazo 9,192.

**CHUO CHA UONGOZI WA FEDHA-CHWAKA**

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Uongozi wa Fedha ni Taasisi ya elimu iliyoanzishwa kwa lengo la kutoa elimu katika fani ya Uongozi wa fedha na fani zinazolingana na mambo ya fedha. Aidha, chuo kinajukumu la kutoa huduma za kiushauri wa kitaalamu na kufanya tafiti. Sambamba na hilo, Chuo kina jukumu la kugundua mahitaji ya mafunzo mafupi katika fani mbali mbali ili kuleta ufanisi katika jamii. Chuo tangu kuanzishwa kwake kimekua kikitoa mafunzo ya ngazi ya cheti, stashahada na shahada katika ya fani ya fedha na fani zinazolingana, zikiwemo Uhasibu, Fedha na Benki, Manunuzi na Ugavi na *TEHAMA* na Uhasibu. Aidha, Chuo kinatoa mafunzo katika ngazi ya stashahada ya Uzamili katika fani ya Uongozi wa fedha katika uhasibu.

Mhe. Naibu Spika, Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015, Chuo kimepata mafanikio yafuatayo: kimeweza kuanzisha shahada ya kwanza katika fani za *TEHAMA* na Uhasibu, Ununuzi na Ugavi , Fedha na Benki na Stashahada ya Uzamili katika fani ya Uhasibu; kimeweza kuongeza idadi ya wanafunzi waliohitimu kwa mafunzo ya ngazi ya cheti, stashahada na shahada kutoka 167 mwaka 2010 hadi kufikia 606 mwaka 2014. Jumla ya wanafunzi elfu mbili mia nane na saba (2807) wamehitimu katika kipindi cha miaka mitano. Hali hii imesaidia kuondoa tatizo la wahasibu wa kada ya kati nchini; Chuo pia kimeimarisha majengo kwa kuongeza vyumba vya kujifunzia kutoka tisa mwaka 2010 hadi kumi na tatu (13) mwaka 2015. Aidha, Chuo kimeweza kujenga dahalia kubwa na ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi mia nne themanini (480) kwa wakati mmoja. Chuo kimesomesha wafanyakazi wanne (4) wa kada ya ualimu) katika shahada ya uzamivu (*PhD*). na wanane(8) masomo ya shahada ya uzamili katika fani mbalimbali kwa fedha za ndani.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo kilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya TZS 1,986.05 milioni kutokana na ada na huduma inazozitoa na kupokea jumla ya TZS 1,800.00 milioni ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini. Hadi kufikia mwezi wa Mei 2015, Chuo kimekusanya kiasi cha TZS 1,641 milioni kutokana na ada za masomo na huduma nyenginezo, sawa na asilimia 82.6 ya

makadirio na kimepokea ruzuku ya TZS 902.00 milioni sawa na aslimia 50 ya makadirio.

**MAMLAKA YA MAPATO (*TRA*)-TAWI LA ZANZIBAR**

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Mapato (*TRA*) kwa upande wa Zanzibar inajukumu la kukusanya mapato yatokanayo na vianzio vya Ushuru wa Forodha, Ushuru wa Bidhaa na Kodi ya Mapato ya Kampuni na Watu binafsi

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya *TRA* ya Zanzibar ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS 166,056.0 milioni katika mwaka wa Fedha wa 2014/2015. Kati ya fedha hizo, Idara ya Forodha ilipangiwa kukusanya TZS.110,553.00 milioni na Idara ya Kodi za ndani ilipangiwa kukusanya TZS 55,502.90 milioni. Hadi kufikia mwezi wa Mei 2015, Ofisi imekusanya TZS 130,045.43 milioni sawa na asilimia 78 ya makadirio ya mwaka. Mapato haya yameongezeka kwa TZS 7,803.74 milioni, kutoka katika kipindi cha Julai mpaka Mei cha mwaka wa Fedha uliopita wa 2013/2014 ambapo *TRA* ilikusanya TZS 122,241.69 milioni. Ongezeko hilo ni sawa na ukuaji wa asilimia 6.4. Fedha zilizokusanywa na Idara ya Forodha ni TZS 80,012.51 milioni na Idara ya Kodi za ndani ilikusanya TZS 46,015.4 milioni.

Mhe. Naibu Spika, Kwa kipindi cha miaka mitano kutoka mwaka 2010 hadi 2015, Mapato yaliyokusanywa na taasisi hii yameongezeka kwa TZS 53,713.00 milioni kutoka TZS 76,333.00 milioni zilizokusanywa katika mwaka 2010. Sababu zilizopelekea mafanikio haya ni:

Kuimarika kwa sekta mbali mbali za uchumi ikiwemo sekta ya mawasiliano, utalii, biashara na ujenzi; Kuimarisha matumizi ya mfumo wa mawasiliano ya habari; Kuimarika kwa mfumo wa kutoa huduma kwa walipa kodi na wadau wengine; Kuimarika kwa huduma ya utoaji elimu wa masuala ya kodi kwa njia ya semina, vipeperushi, vijarida pamoja na kuimarika kwa ulipaji kodi kwa mashirika ya Serikali yakiwemo *ZSTC*, *PBZ*, *ZPC* na *ZIC*.Kiambatanisho nam. 7 kinahusika.

**B. MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016**

Mhe. Naibu Spika, Bajeti ya Wizara ya Fedha ya mwaka wa fedha 2015/16 itatekelezwa kwa kuzingatia misingi mikuu ifuatayo; Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA II), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, Malengo ya Maendeleo ya Milenia (*MDGs*), Sheria na Sera zinazohusiana na masuala ya fedha pamoja na maelekezo kutoka Serikalini.

a. Makadirio ya mapato ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2015/2016

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Fedha inatarajia kukusanya jumla ya mapato ya ndani TZS 467,366.48 milioni kutoka vianzio vya *TRA, ZRB* pamoja na Idara zake. Kwa upande wa mapato kutoka kwa washirika wa maendeleo, Wizara inatarajia kupokea jumla ya TZS 349,876.15 milioni kama zinavyoonekana katika Kiambatanisho nam. 7. Mapato hayo ni ongezeko la asilimia ishirini na nne (24) ikilinganishwa na mapato yaliyokadiriwa kukusanywa kwa mwaka 2014/15.

b. Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2015/2016

Mhe. Naibu Spika, Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 imekusudia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. Kushajihisha na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya TZS 817,242.64 milioni;
ii. Kuanza ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Wizara ya Fedha-Pemba;
iii. Kukamilisha utungaji na kufanya mapitio ya sheria tano (5) za sekta ya fedha ili kuendeleza sekta ya fedha ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa fedha za umma;
iv. Kufanya tafiti mbili (2) kubwa za kitaifa za sekta ya fedha;
v. Kusimamia upatikanaji wa gawio la TZS 5,000.00 milioni kutoka katika Mashirika ya Umma;
vi. Kulipa fidia kwa waathirika wa mradi wa ujenzi wa michirizi unaotekelezwa chini ya mradi wa huduma za jamii mijini, yaani *ZUSP*;
vii. Kukamilisha uanzishwaji wa utumiaji wa risiti za elektroniki;
viii. Kuanzisha kitengo maalum kitakachosimamia mapato ndani ya Wizara;
ix. Kukamilisha ufungaji wa toleo jipya la *IFMS* (*epicor 10*) na kufanya matayarisho ya awali ya ufungaji wa mfumo wa kutoa taarifa za madeni (*CS-DRMS*); pamoja na
x. Kuendelea na shughuli zake za kawaida.

c. Makadirio ya matumizi kwa mwaka 2015/2016

Mhe. Naibu Spika, Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2015/2016 yametayarishwa katika mfumo wa kiprogramu (*Programme Based Budget-PBB*). Katika mfumo huu wa *PBB*, Wizara imeandaa Programu kuu tatu (3) zitakazotekelezwa kupitia programu ndogo nane (8) chini ya fungu F01 na programu kuu moja

itakayotekelezwa chini ya fungu F02 (Mfuko Mkuu wa Serikali). Programu kuu ni hizi zifuatazo:

**Fungu F01-Wizara ya Fedha:**

I. Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma,
II. Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma,
III. Mipango na Uendeshaji wa Sekta ya Fedha

**Fungu F02-Mfuko Mkuu wa Serikali:**

I. Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali.

Wizara inatarajia kutumia jumla ya TZS 155,747.70 milioni kwa ajili ya kutekeleza programu hizo. (Viambatanisho namba XVI hadi XX vinahusika)

**I. Programu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma.**

Mhe. Naibu Spika, Matarajio ya matokeo ya programu hii ni kupatikana ufanisi wa huduma za fedha za Umma. Programu hii inakadiriwa kutumia jumla ya TZS 43,597.32 milioni na itatekelezwa kupitia programu ndogo tatu zifuatazo; Mfumo wa udhibiti na ulipaji; Usimamizi wa Bajeti ya Serikali na; Ufuatiliaji na uratibu wa misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**i. Mfumo wa Udhibiti na Ulipaji**

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Mfumo wa Udhibiti na Ulipaji ina lengo la kuimarisha mfumo wa malipo ili kwenda sambamba na viwango vya kimataifa. Matarajio ya programu hii ni kuhakikisha matumizi ya fedha za umma yanafanyika kwa kufuata taratibu zilizoanishwa katika sheria ya fedha. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni; Utoaji wa fedha kwa Wizara na taasisi kwa wakati, kuandaa na kutoa taarifa za fedha kwa mwaka, Kutoa ushauri wa masuala ya fedha kwa Wizara na taasisi za Serikali, Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na kusimamia utoaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara. Programu ndogo hii itatekelezwa na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na inakadiriwa kutumia jumla ya TZS 26,221.40 milioni.

**ii. Usimamizi wa Bajeti ya Serikali**

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Usimamizi wa bajeti ya Serikali lengo lake ni kusimamia na kutayarisha bajeti ya Serikali. Matokeo ya programu ni kuhakikisha kuwepo mgawanyo wa rasilimali unaozingatia vipaumbele vya Taifa kwa sekta mbali mbali za Serikali. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni

Utayarishaji na ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti, Kutoa taaluma ya bajeti kwa jamii na taasisi za Serikali pamoja  na kutoa taarifa za mishahara ya wafanyakazi wa Serikali. Programu ndogo hii itatekelezwa na Idara ya Bajeti na makadirio ni kutumia jumla ya TZS 15,588.24 milioni.

**iii. Ufuatiliaji na uratibu misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya ufuatiliaji na uratibu wa misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ina lengo la kuimarisha ufuatiliaji na upatikanaji wa misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Matokeo ya programu hii ni kupata fedha zitakazotumika kuimarisha miundombinu; barabara, kumalizia ujenzi wa jengo la Abiria Uwanja wa Ndege wa Zanzibar,maji na umeme, miradi ya elimu ya msingi, kati na vyuo vya amali, kuimarisha afya pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Huduma zitakazotolewa  ni Uimarishaji wa utafutaji kwa ufuatiliaji wa fedha (misaada na mikopo) kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, uratibu wa mashirikiano na Washirika wa Maendeleo pamoja na Ushajiishaji wa upatikanaji wa rasilimali fedha.

Programu hii inatarajiwa kutekelezwa na Idara ya Fedha za nje. Programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya TZS 1,787.68 milioni katika utekelezaji wake.

**II. Programu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma.**

Mhe. Naibu Spika, Matarajio ya matokeo ya programu hii ni kuwa na mfumo bora wa kusimamia mali za Umma na uwekezaji wake. Utekelezaji wa programu hii utasimamiwa na Idara ya Uhakikimali na Mitaji ya Umma. Aidha, utekelezaji wa program hii utapitia katika programu ndogo mbili (2) ambazo ni; Usimamizi wa Mitaji ya Umma na Usimamizi wa Manunuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali.

**i. Usimamizi wa Mitaji ya Umma**

Mhe. Naibu Spika, lengo kuu la programu ndogo ya usimamizi wa mitaji ya umma ni kusimamia mitaji inayowekezwa katika mashirika ya Serikali na hisa zinazowekezwa katika makampuni mbali mbali. Matokeo ya programu hii ni kupatikana ufanisi wa kiutendaji utakaowezesha mashirika hayo kuimarika kiuchumi na hatimae kuchangia maendeleo ya nchi. Huduma zitakazotolewa na programu ndogo hizi ni Usimamizi na tathmini ya mitaji na hisa za Serikali, Ujenzi wa Ofisi za Serikali pamoja na ushajiishaji wa wawekezaji wa nje na ndani.

**ii. Usimamizi wa Manunuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali**

Mhe. Naibu Spika, lengo kuu la programu hii ndogo ni kuwepo kwa uwazi na usawa wa tathmini ya bidhaa zinazonunuliwa katika taratibu za manunuzi. Matokeo ya programu hii ni kupatikana uwajibikaji na uwazi utakaopelekea kuimarika kwa utawala bora nchini. Huduma zitakazotolewa ni usimamizi wa manunuzi ya mali kwa Wizara na taasisi za Serikali na uhakiki wa mali za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma utekelezaji wake utasimamiwa na Idara ya Uhakikimali na Mitaji ya Umma. Kwa ujumla,programu hii inakadiriwa kutumia TZS 2,250.68 milioni.

**III. Program ya Mipango na Uendeshaji wa Sekta ya Fedha**

Mhe. Naibu Spika, Matokeo ya programu hii ni kuwa na sekta ya Fedha iliyoimara itakayosaidia kukuza uchumi wa nchi. Programu hii imeundwa na programu ndogo tatu (3) ambazo ni; Utawala na Uendeshaji wa Wizara, Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Wizara-Pemba pamoja na Mipango, Sera na tafiti za sekta ya fedha. Jumla ya TZS 26,351.0 milioni zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii.

**i.Utawala na Uendeshaji wa Wizara**

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara lengo lake kuu ni kuweka mazingira bora kwa wafanyakazi. Matokeo ya programu hii ni ufanisi katika kazi za Wizara na taasisi zake. Huduma zitakazotolewa ni Usimamizi na utoaji wa huduma za kiutumishi, kuimarisha huduma za *TEHAMA* ndani ya Wizara na Utoaji wa mafunzo ya fani zinaoendana na usimamizi wa fedha na mali za Serikali. Idara ya Utawala na Uendeshaji itasimamia utekelezaji wake na inakadiriwa kutumia jumla ya TZS 5,281.50 milioni.

**ii. Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Wizara-Pemba**

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Uratibu wa utekelezaji wa shughuli za Wizara-Pemba ina lengo la kupatikana ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba. Matarajio ya programu hii ni kuimarika kwa huduma za sekta ya fedha kwa upande wa Pemba. Programu ndogo hii itatekelezwa chini ya usimamizi wa Ofisi kuu ya Wizara-Pemba na inakadiriwa kugharimu jumla ya TZS 1,238.19 milioni.

### iii. Mipango, Sera na tafiti za sekta ya Fedha

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Mipango, Sera na tafiti za sekta ya Fedha itasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Lengo lake kuu ni kuimarisha sekta ya fedha itakayokwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi. Matokeo ya programu hii ni kuwa na sekta ya fedha iliyo imara na itakayohimili mabadiliko ya kiuchumi duniani. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kufanya tafiti, Uandaaji wa Sera, Sheria na Mipango itakayosaidia ukuaji wa sekta ya Fedha, usimamizi na uendeshaji wa mijadala ya utatuzi wa migogoro ya kodi, utayarishaji wa mpango mkuu wa maeneo huru-Fumba pamoja na kuimarisha huduma za jamii mijini. Jumla ya TZS 19,831.32 milioni zimekadiriwa kutumika katika ufanikishaji wa programu ndogo hii

### IV.Programu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali

Mhe. Naibu Spika, Lengo kuu la programu hii ni kuhakikisha matumizi maalum ya Serikali yanafanyika kwa ufanisi pamoja na kufuata taratibu za kisheria. Matokeo ya programu hii ni kuhakikisha matumizi maalum ya Serikali yanafanyika kwa kuzingatia utaratibu uliopangwa na kwa wakati. Huduma zinazotarajiwa kutolewa kupitia programu hii ni kufanya malipo ya gharama za matukio yasiotarajiwa pamoja na kufanya malipo ya matumizi maalum ya Serikali yakijumuisha malipo ya Viinua mgongo, pencheni, madeni na matumizi mengineyo ya Serikali. Jumla ya TZS 83,548.70 milioni zinakadiriwa kutumika kwa ajili ya utekezaji wa programu hii.

## C. MUELEKEO WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA MWAKA 2015/2016

BODI YA MAPATO ZANZIBAR (*ZRB*)

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Bodi ya Mapato Zanzibar itatekeleza malengo makuu yafuatayo; Kukusanya jumla TZS. 250,900.00 milioni kutokana na vyanzo vya kodi na visivyo vya kodi; Kuendelea kuimarisha miundombinu ya mtandao wa mawasiliano (*ICT*) na utendaji kazi; Kushajiisha ulipaji kodi wa hiari na kutoa huduma bora kwa walipakodi; na Kuweka mazingira bora ya kufanya kazi kwa kununua vitendeakazi na kuwajengea uwezo watendaji katika masuala ya fedha, kodi, Sheria, *TEHAMA* na utawala kwa kuwadhamini katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Taasisi hii imekadiriwa kupatiwa ruzuku ya jumla ya TZS. 11,300.00 milioni kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake.

## MFUKO WA BARABARA

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa Fedha wa 2015/2016 Mfuko unalenga kupokea makusanyo ya jumla ya TZS 10,227.37 milioni, kati ya hizo TZS 9,046.00 milioi zikiwa ni makusanyo yatokanayo na *Roads Development Levy* na TZS 6.37million kutokana na ukodishaji wa jengo na TZS 1,175.00 milioni kutokana na tozo ya uingizaji magari "*Motor Vehicle Levy*". Kati ya fedha hizo jumla ya TZS 8,991.00 milioni zitatumika kwa kazi za matengenezo ya barabara.

Mhe. Naibu Spika, Kuanzia mwaka wa fedha wa 2015/2016, asilimia themanini na tano (85) ya fedha za matengenezo ya barabara zitagaiwa kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kufanya matengenezo ya kawaida ya kusafisha na kuziba viraka barabara zote za lami, kufanya matengenezo ya barabara kwa kiwango cha lami kilomita 17, kufanya matengenezo ya barabara za kifusi 43 kilomita, kuweka taa za kuongozea magari sehemu nne tofauti. Aidha, asilimia 15 zitapelekwa kwa Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ambao kimsingi wana jukumu la kutunza barabara za ndani ambapo kwa mwaka 2015/2016 itatekeleza ujenzi wa barabara wa 7.5 kiliomita. Hata hivyo bado Mfuko wa Barabara utakuwa na wajibu wa kuzisimamia fedha hizo.

## MAMLAKA YA UWEKEZAJI NA VITEGA UCHUMI

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa Fedha 2015/2016, Mamlaka inakusudia kukusanya jumla ya TZS 3,402.77 milioni ambapo TZS 1,564.44 milioni kutoka vyanzo vya ndani, TZS 1,138.34 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 250.00 milioni ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Mamlaka imepanga kutekeleza yafuatayo: Kuendeleza ujenzi wa miundombinu katika maeneo huru ikiwa ni hatua za kuendeleza mpango wa kuanzisha mji wa biashara (*Fumba Bay Satellite City*); Kuendeleza ujenzi wa mji mdogo wa kibiashara Nyamanzi chini ya usimamizi wa Mamlaka na Kampuni binafsi; Kushajihisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika sekta za uvuvi wa bahari kuu, ujenzi wa nyumba za kibiashara (*real estate)* na utalii kwa upande wa ujenzi wa kumbi za mikutano ya kimataifa (*conventional village*) kwa nia ya kuendeleza juhudi za Serikali katika kuinua uchumi.

Juhudi hizo zinalenga masoko yanayochipukia kutoka nchi za Uturuki, Urusi, China na India; Kuendelea na tafiti mbali mbali ikiwemo Utafiti wa Mwenendo wa Mitaji Binafsi (*PCF*) ili kutambua fursa mpya za wawekezaji na jinsi ya kuinua wajasiriamali na Kuelimisha jamii juu ya umuhimu na faida zinazopatikana katika uwekezaji.

## CHUO CHA UONGOZI WA FEDHA-CHWAKA

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Chuo kimekadiria kukusanya jumla ya TZS 2,521.29 milioni kutokana na ada na huduma zinazotolewa. Aidha, Chuo kinatarajia kupokea ruzuku ya TZS 1,344.00 milioni kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa kazi za kawaida.

Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Chuo kinatarajia kutekeleza mambo makuu yafuatayo: Kufundisha na kutahini wanafunzi 1300 katika fani za Uongozi wa Fedha, *TEHAMA* na Uhasibu, Ununuzi na Ugavi pamoja na Fedha na Benki katika ngazi za cheti, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili.

Aidha, Chuo kina dhamira ya kuanzisha Shahada ya Uzamili katika fani ya ukaguzi na ushauri (*MSc in Auditing and Consultancy);* Kuandika na kuandaa maandiko ya utafiti pamoja na kufanya tafiti ndogo ndogo za kusaidia kutatua kero zinazozikabili jamii na Serikali kwa ujumla na Kutoa ushauri elekezi kwa taasisi binafsi, Serikali na kutoa elimu za kiuchumi na fedha kwa jamii katika ngazi ya wilaya.

## MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (*ZSSF*)

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Mfuko unatarajia kufanya kazi zifuatazo; Kukusanya michango ya wanachama ya TZS 44,148.00 milioni kutoka kwa wanachama Serikalini, Mashirika ya Umma na Taasisi binafsi; Kuendelea kulipa mafao ya TZS 11,831.00 milioni kwa wanachama 5,379; Kufanya uwekezaji wa jumla ya TZS 16,528.00 milioni katika maeneo ya muda mrefu na yale ya muda mfupi; Kwa upande wa miradi ya ujenzi, Mfuko umepanga kuanza ujenzi wa nyumba za kisasa eneo la Mbweni, ujenzi ambao kwa awamu ya kwanza unatarajiwa kugharimu jumla ya TZS 10,000.00 milioni; Kuanza matayarisho ya ujenzi wa jengo la biashara (*Shopping Mall)* eneo la Michenzani makontena, ujenzi ambao kwa hatua ya awali unatarajiwa kugharimu jumla ya TZS 8,500.00 milioni. Kwa ujumla Mfuko umepangiwa kutumia katika miradi ya ujenzi jumla ya TZS 22,400.00 milioni kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

## BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (*PBZ*)

Mhe. Naibu Spika, Benki ya Watu wa Zanzibar imekusudia kutekeleza majukumu yake makuu ya kukusanya amana za wateja ambapo kwa mwaka 2015/2016 imekadiria kukusanya jumla ya TZS 381,000.00 milioni na kutoa mikopo yenye thamani TZS 235,090.00 milioni. Aidha, *PBZ* inatarajia kukusanya TZS

44,000.00 milioni kutoka katika vianzio mbali mbali vya mapato. Katika kuongeza wigo wa kutoa huduma, *PBZ* inatarajia kufungua tawi katika Mkoa wa Mtwara, kuongeza tawi jipya maeneo ya *TAZARA* Jijini Dar es Salaam, Kujenga tawi kwa ajili ya kutoa huduma kwa wateja wakubwa maeneo ya Malindi kiwanja cha Shirika la Magari. Benki inatarajia kuanzisha vituo vya huduma Kiwengwa na Nungwi kwa upande wa Unguja na Wete kwa upande wa Pemba ili kutoa huduma za Benki ya Kiislam na kuanzisha huduma za Benki kupitia Mawakala "*Agency Banking*".

SHIRIKA LA BIMA

Mhe. Naibu  Spika, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Shirika la Bima linaendelea kutekeleza majukumu yafuatayo: Kutoa huduma bora na za kisasa; Kuongeza mapato ya Shirika kwa asilimia 15; Kuongeza faida kwa mmiliki wa Shirika; Kuongeza uwekezaji wenye faida kwa Shirika; Kuwezesha Shirika kutumia teknolojia ya kisasa katika kutoa huduma zake; Kuongeza wigo wa soko *(Market Share)* kwa asilimia 5; Kushiriki katika kusaidia huduma za kijamii.

Mhe. Naibu  Spika, Katika kipindi cha mwaka 2015/2016, Shirika linakadiria kukusanya jumla ya TZS.19, 287.00 milioni kutokana na vianzio mbali mbali vya mapato. Kulingana na makadirio hayo, mapato yatakuwa yamepanda kwa asilimia 10 ukilinganishwa na mapato halisi ya mwaka uliopita. Kwa upande wa matumizi, Shirika linatarajia kutumia jumla ya TZS.5,483.00 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 1,527.00 milioni kwa kazi za maendeleo.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (*TRA*)-TAWI LA ZANZIBAR

Mhe. Naibu  Spika, Kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) tawi la Zanzibar imepangiwa kukusanya TZS. 178,563.34 millioni sawa na ongezeko la asilimia 7.5 ya makadirio ya makusanyo ya TZS 166,100.00 millioni ya mwaka wa fedha 2014/2015. Kati ya makadirio hayo Idara ya Forodha imepangiwa kukusanya TZS.113, 845.64 milioni sawa na asilimia 64 ya makadirio ya mwaka na Idara ya Kodi ya ndani imepangiwa kukusanya TZS 64,717.67 millioni sawa na asilimia 36 ya makadirio.

**SHUKRANI**

Mhe. Naibu  Spika, Kwa nafasi ya pekee nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake uliojaa hekima na busara ambao umetuwezesha kupiga hatua kubwa katika Maendeleo ya nchi yetu. Naomba tena pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kuniamini

kushika dhamana hii kwa kipindi chote cha miaka mitano ya uongozi wake wa awamu ya saba. Mheshimiwa Rais, ninaamini kwamba hekima, busara na miongozo uliyotupatia ni nyenzo kuu ambazo tumezitumia na tutaendelea kuzitumia ili kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Natoa shukurani zangu kwako wewe binafsi, Kamati za kudumu za Baraza lako pamoja na Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa ushirikiano mzuri tunaoendelea kuupata katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha. Aidha, napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa mashirikiano yao mema na kwa misaada yao wanayoendelea kuitoa ili kuiwezesha na kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha Uchumi wake. Mashirika haya yanajumuisha, Benki ya Maendeleo ya Afrika; Benki ya Dunia; Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika; Umoja wa Ulaya; *IFAD*; *OPEC* na Taasisi za Umoja wa Mataifa; Serikali ya Marekani (*USA*); Sweden; Norway; Denmark; China; Nertherland; Spain, Saudi-Arabia pamoja na Japani. Pia, naomba kuzishukuru Taasisi na wananchi wote kwa ujumla kwa kunisikiliza kwa makini wakati nikiwasilisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wote wa Wizara ya Fedha, unaoongozwa na Ndugu Khamis Mussa Omar, Katibu Mkuu na Ndugu Juma A. Hafidh Naibu Katibu Mkuu na Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa umahiri wao wanaounyesha katika ufanisi wa kazi za Wizara. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara na Taasisi pamoja na Wafanyakazi wote kwa michango na ushirikiano wao mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii yenye umuhimu wa pekee katika Serikali.

## HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mbele ya Baraza lako tukufu, juu ya hali ya utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara ya Fedha na Taasisi zake, naomba nihitimishe kwa kutoa matarajio ya jumla katika utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka ujao wa 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara ya Fedha inatarajia kuendelea kuimarisha uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kiwango cha asilimia 21.1 ya pato la Taifa na kusimamia vyema matumizi ya rasilimali zitakazokusanywa. Katika kulitekeleza suala hili, Wizara imekusudia kuanzisha kitengo maalum ndani ya Wizara kitakachoshughulikia mapato ya Serikali pamoja na kukiimarisha kitengo cha ukusanyaji wa taarifa za mapato.

Aidha, Wizara inaendelea na maandalizi ya matumizi ya mashine za kutolea risiti kwa wafanya biashara, sambamba na hilo Wizara inaendelea kuimarisha mifumo

inayotumika katika ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya fedha za Umma pamoja na kutoa taaluma kwa watumiaji wa mifumo hiyo. Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Rufaa ya kodi itaendelea kusikiliza na kutatua migogoro ya kodi ili kuhakikisha kunapatikana haki na uwazi baina ya Serikali na walipakodi. Wizara itahakikisha kuwa kuna usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa mapato kwa Taasisi zote ili kuhakikisha malengo waliyowekewa yanafikiwa. Usimamizi huo utajumuisha kuzipitia mara kwa mara Taasisi husika kwa kuzifanyia tathmini na kuzikagua, ili kujua changamoto zilizopo kwa lengo la kuimarisha vyanzo vya ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Naibu  Spika, Naomba kuchukua nafasi hii kuwakumbusha Wakuu wa Taasisi za ukusanyaji kuwa wawe makini katika kusimamia mapato ya Taasisi zao ili kufanikisha shabaha zilizowekwa.

Mhe.Naibu Spika, Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/2016, Wizara imejiandaa kusimamia upatikanaji wa kodi iliyokusudiwa kuchangia Mfuko maalum wa Miundombinu pamoja na kufatilia matumizi yatakayofanywa kupitia Mfuko huo. Mkakati huu umepangwa baada ya kuonekana kwamba ujenzi wa miundombinu ulikuwa ukitegemea zaidi kupokea fedha kutoka kwa Washirika wa maendeleo, ambapo kwa sasa mwenendo wa upatikanaji wa fedha hizo umekuwa sio wa kuridhisha kutokana na sababu mbali mbali zinazoibuliwa na Washirika hao. Aidha, Wizara imeshajiandaa kutekeleza dhamira mpya ya Serikali ya kuwapatia mafao wazee wote waliofikia umri wa miaka 70. Dhamira hii ni ya kipekee kwa Afrika Mashariki na Kati. Utekelezaji huu utakwenda sambamba na kuongeza kiwango cha pencheni kwa wastaafu wa Serikali.

Mhe.Naibu Spika, Naomba kulithibitishia Baraza lako tukufu kwamba, kutokana na umuhimu wa matumizi ya barabara zetu katika kuendesha shughuli za kiuchumi, Wizara itafuatilia kwa umakini mkubwa fedha zilizopangwa kuchangia Mfuko wa barabara na kuhakikisha fedha hizo zinafika katika Mfuko kwa wakati ili kuharakisha matengenezo ya Barabara zetu.

Mhe. Naibu  Spika, Kwa mara nyengine tena naomba nichukue fursa hii adhimu kuzungumzia umuhimu wa amani katika nchi yetu. Amani na Utulivu ni nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo endelevu ya nchi hii; kama tunavyotambua kwamba ghasia na migogoro katika nchi ni kikwazo kikubwa cha maendeleo.

Mhe. Naibu  Spika, Naomba nikumbushie kwamba, kwa kipidi cha miaka mitano cha uongozi wa awamu ya saba, tumeshuhudia Maendeleo makubwa yaliyofikiwa na nchi yetu. Maendeleo hayo yaliyopatikana yametokana na busara, hekima tulizonazo pamoja na kuwa na amani na utulivu nchini. Aidha, naomba tuelewe

kwamba nchi yetu ni ya kidemokrasia, na katika mwaka huu kama ulivyo utaratibu tunakabiliwa na uchaguzi mkuu.


Napenda kuihusia nafsi yangu pamoja na kuwasihi wananchi wote kwa ujumla kwamba, tusikubali kugaiwa kwa kutumia misingi yetu ya imani pamoja na siasa zetu ili kuvuruga amani ya nchi yetu. Amani haichezewi, wala amani haina bei, hivyo, inatupasa muda mwingi kufikiria yale yanayotuunganisha, ni muhimu zaidi kuliko yale yanayotugawa na kutusambaratisha. Kwa pamoja tunawajibu wa kulinda amani iliyopo pamoja na mashirikiano yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala*, atuzidishie umoja na mshikamano ili tuweze kuitunza amani hii na kudumisha utulivu tulionao nchini mwetu daima, *Amin* na huu mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Naibu Spika, Baada ya maelezo hayo sasa naliomba baraza lako tukufu likae kama kamati ili kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha matumizi ya jumla ya TZS 155,747.70 milioni ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2015/2016.
Mhe. Naibu Spika, Naomba kutoa hoja.

**Viambatanisho vya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka**

**2014-2015**

**Kiambatanisho namba I**





**Chanzo:** Wizara ya Fedha-Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

**Kiambatanisho namba II**

| Matumizi ya Wizara kwa kipindi cha Julai 2014-Mei 2015 | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| **Maelezo** | **Makadirio TZS"000,000** | **Halisi TZS"000,000** | **Asilimia %** |
| **Matumizi ya kawaida:** | | | |
| Mshahara | 9,290.22 | 4,342.93 | 47% |
| Ruzuku | 17,452.30 | 15,023.00 | 86% |
| Matumizi Mengineyo | 5,044.15 | 4,434.55 | 88% |
| Matumizi ya Mfuko Mkuu | 69,800.00 | 58,250.37 | 83% |
| **Jumla ndogo(a)** | **101,586.67** | **82,050.85** | 81% |
| | | | |
| **Matumizi ya kazi za Maendeleo:** | | | |
| Mchango wa Serikali | 27,203.00 | 21,869.86 | 80% |
| Fedha kutoka kwa Washirika wa | 14,293.50 | 8,500.00 | 59% |
| **Jumla ndogo (b)** | **41,496.50** | **30,369.86** | **73%** |
| **Jumla kuu (a +b)** | **143,083.17** | **112,420.71** | **79%** |


Chanzo: Wizara ya Fedha-Idara ya Utawala na Uendeshaji.

**Kiambatanisho namba III**




**Chanzo: Wizara ya Fedha-Idara ya Mipango, Sera na Utafiti**

**Kiambatanisho namba IV**




Chanzo: Wizara ya Fedha-Idara ya Bajeti

**Kiambatanisho namba V**

| **Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka Julai 2014-Mei 2015** | | | |
|---|---|---|---|
| **Tarakimu ni TZS "000,000"** | | | |
| | | | |
| **Maelezo;** | **Makadirio** | **Halisi** | **%** |
| **Mapato ya ndani;** | | | |
| Bodi ya Mapato (ZRB) | 181,300.00 | 160,829.00 | 89% |
| Mapato yasikuwa ya kodi | 18,400.00 | 18,500.00 | 101% |
| Mamlaka ya Mapato-TRA | 166,100.00 | 130,045.00 | 78% |
| PAYE Kutoka SMT | 21,000.00 | 19,250.00 | 92% |
| Mikopo ya kibenki | 15,000.00 | 10,072.00 | 67% |
| **Jumla ndogo (A)** | **401,800.00** | **338,696.00** | 84% |
| **Mapato kuoka Nje:** | | | |
| Misaada ya Kibajeti(GBS) | 40,000.00 | 16,338.00 | 41% |
| MDRI | 600.00 | 769.64 | 128% |
| Mapato kutoka kwa Washirika w | 265,400.00 | 83,313.74 | 31% |
| **Jumla ndogo (B)** | **306,000.00** | **100,421.38** | 33% |
| **Jumla kuu ya Mapato (A+B)** | **707,800.00** | **439,117.38** | 62% |
| | | | |
| **Matumizi;** | | | |
| Mshahara | 184,500.00 | 166,816.00 | 90% |
| Matumizi Mfuko Mkuu | 69,800.00 | 58,250.00 | 83% |
| Ruzuku | 50,400.00 | 39,745.00 | 79% |
| Matumizi Mengineyo | 71,800.00 | 51,118.00 | 71% |
| **Jumla ndogo( C )** | **376,500.00** | **315,929.00** | 84% |
| **Matumizi kazi za Maendeleo;** | | | |
| Mchango wa Serikali | 65,900.00 | 41,998.00 | 64% |
| Washirika wa Maendeleo | 265,400.00 | **96,137.64** | 36% |
| **Jumla ndogo ( D )** | **331,300.00** | **138,135.64** | 42% |
| **Jumla kuu ya Matumizi( C + D** | **707,800.00** | **454,064.64** | 64% |


**Chanzo;** Wizara ya Fedha-Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali

**Kiambatanisho namba VI.**

Mapato yaliyokusanywa na Bodi ya Mapato 2010-2015

Tarakimu ni milioni TZS

| Mwaka | Makadirio | Makusanyo | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2010/11 | 91,735.34 | 92,364.72 | 101% |
| 2011/12 | 109,644.05 | 109,642.51 | 100% |
| 2012/13 | 146,000.00 | 129,926.19 | 89% |
| 2013/14 | 154,668.00 | 156,572.33 | 101% |
| 2014/15 | 181,300.00 | 160,829.00 | 89% |





Chanzo; Bodi ya Mapato-Zanzibar.

**Kiambatanisho namba VII**

Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato(TRA) 2010-2015

Tarakimu ni milioni TZS


| Mwaka | Makadirio | Makusanyo | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2010/11 | 69,240.74 | 76,332.87 | 110% |
| 2011/12 | 100,580.91 | 100,579.00 | 100% |
| 2012/13 | 106,731.00 | 103,936.12 | 97% |
| 2013/14 | 146,306.00 | 136,720.07 | 93% |
| 2014/15 | 166,100.00 | 130,045.00 | 78% |




Chanzo; TRA-Zanzibar

**Kiambatanisho namba VIII**

| **Mapato yasiokuwa ya kodi kwa Serikali 2010-2015** | | | |
|---|---|---|---|
| | **Tarakimu ni milioni TZS** | | |
| Mwaka | Makadirio | Makusanyo | Asilimia |
| 2010/11 | 10,711.40 | 12,786.58 | 119% |
| 2011/12 | 11,014.97 | 11,460.28 | 104% |
| 2012/13 | 20,000.00 | 11,781.96 | 59% |
| 2013/14 | 16,400.00 | 14,617.10 | 89% |
| 2014/15 | 18,400.00 | 18,500.00 | 101% |





**Chanzo: Mhasibu Mkuu wa Serikali**

## Kiambatanisho namba IX

Mwenendo wa Mapato ya ndani yaliyokusanywa kwa kipindi cha mwaka 2010- Mei 2015


Tarakimu ni milioni-TZS

| Maelezo: | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 |
|---|---|---|---|---|---|
| Bodi ya Mapato(ZRB) | 92,364.00 | 108,879.00 | 129,926.00 | 156,572.00 | 160,829.00 |
| Mamlaka ya Mapato (TRA) | 76,332.00 | 91,694.00 | 103,936.00 | 136,720.00 | 130,045.00 |
| Mapato yasiyokuwa ya kodi (bila ya Gawio la BOT) | 12,786.00 | 11,460.00 | 11,781.00 | 14,617.00 | 15,300.00 |
| Gawio | - | 7,796.00 | - | 1,805.00 | 3,200.00 |
| Kodi ya wafanyakazi kutoka SMT | - | - | 21,000.00 | 21,000.00 | 19,250.00 |
| **Jumla ya Mapato ya ndani (a)** | **181,482.00** | **219,829.00** | **266,643.00** | **330,714.00** | **328,624.00** |
| **Makadirio ya Makusanyo ya Mapato ya Ndani(b)** | **171,687.51** | **221,239.93** | **294,131.00** | **350,600.00** | **386,800.00** |
| **Asilimia ya Makusanyo Vs Makadirio (a/b)** | **106%** | **99%** | **91%** | **94%** | **85%** |
| Pato la Taifa ( c ) | 1,050,800.00 | 1,344,100.00 | 1,565,200.00 | 1,849,900.00 | 2,133,500.00 |
| Uwiano wa Mapato ya ndani na Pato la Taifa(c/a) | 17% | 16% | 17% | 18% | 15% |
| Deni la ndani (d) | 36,635.35 | 58,738.34 | 50,202.51 | 85,072.91 | 100,186.31 |
| Uwiano wa Mapato ya ndani na deni la ndani(a/d) | 5:1 | 4:1 | 5:1 | 4:1 | 3:1 |




Chanzo: Wizara ya Fedha-Zanzibar

**Kiambatanisho namba X**




Chanzo; Wizara ya Fedha-Kitengo cha Deni la Taifa

## Kiambatanisho XI.


| ORODHA YA PROGRAMU/MIRADI ILIYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA 2014/2015 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | WIZARA YA FEDHA | | TZS "000" | | | |
| JINA LA MRADI | MAKISIO KWA MWAKA 2014/2015 | | | | MATUMIZI HALISI | | | | |
| | SMZ | MUHISANI | | JUMLA | SMZ | % | MUHISANI | % | JUMLA |
| Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) | 10,000.00 | World Bank | 1,000,000.00 | 1,010,000.00 | 700.00 | 7% | 1,000,000.00 | 100% | 1,000,700.00 |
| Kuimarisha Usimamizi wa Misaada Zanzibar | 10,000.00 | UNDP | 326,000.00 | 336,000.00 | - | | 223,922.00 | 69% | 223,922.00 |
| Program ya Ujenzi wa Afisi za Serikali Zanzibar | 2,157,656.90 | | - | 2,157,656.90 | - | | | | - |
| i) Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko | | | | | | | | | - |
| ii) Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano | | | | | | | | | - |
| iii) Wizara Ya Fedha, | | | | | | | | | - |
| iv) Wizara ya Ustawi wa jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake | | | | | | | | | - |
| v) Wizara ya Katiba na Sheria | | | | | | | | | - |
| vi) Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora | | | | | | | | | - |
| Programu wa Huduma za jamii Mijini (ZUSP) | 1,600,000.00 | World Bank | 10,611,176.00 | 12,211,176.00 | 29,517.00 | 2% | 10,725,190.41 | 101% | 10,754,707.41 |
| Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFM) | 20,000.00 | | - | 20,000.00 | 14,400.00 | 72% | - | - | 14,400.00 |
| Utayarishaji wa mpango mkuu wa maeneo huru Fumba | 150,000.00 | | - | 150,000.00 | 100,000.00 | 67% | - | - | 100,000.00 |
| Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya pili | 10,000.00 | AFDB | 726,325.00 | 736,325.00 | 10,000.00 | 100% | 271,345.19 | 37% | 281,345.19 |
| Programu ya upatikinaji wa rasilimali fedha | 2,403,000.00 | | - | 2,403,000.00 | 868,600.91 | 36% | | | 868,600.91 |
| JUMLA | 6,360,656.90 | | 12,663,501.00 | 19,024,157.90 | 1,023,217.91 | 16% | 12,220,457.60 | 97% | 13,243,675.51 |
| UNUNUZI WA MELI | 20,842,343.10 | | - | 20,842,343.10 | 20,842,343.00 | 100% | - | | 20,842,343.00 |
| JUMLA KUU | 27,203,000.00 | | 12,663,501.00 | 39,866,501.00 | 21,865,560.91 | 80% | 12,220,457.60 | 97% | 34,086,018.51 |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha-Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

**Kiambatanisho namba XII.**

Fedha kutka kwa Washirika wa Maendeleo 2010-2015

| Mwaka | Ruzuku | Mikopo | Jumla ya fedha |
|---|---|---|---|
| 2010/2011 | 51,910.67 | 84,764.59 | 136,675.26 |
| 2011/2012 | 94,905.40 | 110,438.92 | 205,344.31 |
| 2012/2013 | 131,873.61 | 69,483.94 | 201,357.55 |
| 2013/2014 | 60,947.81 | 135,547.51 | 196,495.32 |
| 2014/2015 | 24,695.74 | 58,618.00 | 83,313.74 |





Chanzo; Idara ya fedha za Nje

# Kiambatanisho namba XIII.

| ORODHA YA PROGRAMU/MIRADI ILIYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA 2014/2015 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| WIZARA YA FEDHA TZS "000" | | | | | | | | | |
| JINA LA MRADI | MAKISIO KWA MWAKA 2014/2015 | | | | MATUMIZI HALISI | | | | |
| | SMZ | MUHISANI | | JUMLA | SMZ | % | MUHISANI | % | JUMLA |
| Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) | 10,000.00 | World Bank | 1,000,000.00 | 1,010,000.00 | 700.00 | 7% | 1,000,000.00 | 100% | 1,000,700.00 |
| Kuimarisha Usimamizi wa Misaada Zanzibar | 10,000.00 | UNDP | 326,000.00 | 336,000.00 | - | | 223,922.00 | 69% | 223,922.00 |
| Program ya Ujenzi wa Afisi za Serikali Zanzibar | 2,157,656.90 | | - | 2,157,656.90 | - | | | | - |
| i) Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko | | | | | | | | | - |
| ii) Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano | | | | | | | | | - |
| iii) Wizara Ya Fedha, | | | | | | | | | - |
| iv) Wizara ya Ustawi wa jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake | | | | | | | | | - |
| v) Wizara ya Katiba na Sheria | | | | | | | | | - |
| vi) Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora | | | | | | | | | - |
| Programu wa Huduma za jamii Mijini (ZUSP) | 1,600,000.00 | World Bank | 10,611,176.00 | 12,211,176.00 | 29,517.00 | 2% | 10,725,190.41 | 101% | 10,754,707.41 |
| Programu ya Mageuzi katika usimamizi wa Fedha za Umma (PFM) | 20,000.00 | | - | 20,000.00 | 14,400.00 | 72% | - | - | 14,400.00 |
| Utayarishaji wa mpango mkuu wa maeneo huru Fumba | 150,000.00 | | - | 150,000.00 | 100,000.00 | 67% | - | - | 100,000.00 |
| Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya pili | 10,000.00 | AFDB | 726,325.00 | 736,325.00 | 10,000.00 | 100% | 271,345.19 | 37% | 281,345.19 |
| Programu ya upatikinaji wa rasilimali fedha | 2,403,000.00 | | - | 2,403,000.00 | 868,600.91 | 36% | | | 868,600.91 |
| **JUMLA** | **6,360,656.90** | | **12,663,501.00** | **19,024,157.90** | **1,023,217.91** | **16%** | **12,220,457.60** | **97%** | **13,243,675.51** |
| **UNUNUZI WA MELI** | **20,842,343.10** | | **-** | **20,842,343.10** | **20,842,343.00** | **100%** | **-** | | **20,842,343.00** |
| **JUMLA KUU** | **27,203,000.00** | | **12,663,501.00** | **39,866,501.00** | **21,865,560.91** | **80%** | **12,220,457.60** | **97%** | **34,086,018.51** |

## Kiambatanisho namba XIV

| Mwenendo wa Amana na Mikopo ya Mabenki(TZS Bilioni) 2011-2015 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Machi 2011 | Machi 2012 | Machi 2013 | Machi 2014 | Machi 2015 |
| Amana | 311.9 | 352.1 | 403.4 | 477.7 | 536.8 |
| Mikopo | 100.4 | 146.9 | 151.5 | 203.8 | 205.8 |





Chanzo; OCGS

**Kiambatanisho namba XV.**

Taarifa za Benki ya Watu wa Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitano (2010-2015)

Tarakimu ni milioni-TZS

| Mwaka | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | Mei, 2015 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Amana | 119,004.00 | 140,020.00 | 195,583.00 | 251,460.00 | 337,710.00 | 366,500.00 |
| Mikopo | 33,456.00 | 61,970.00 | 94,866.00 | 137,400.00 | 193,430.00 | 229,700.00 |
| Rasilimali | 142,061.00 | 170,380.00 | 227,926.00 | 287,750.00 | 382,050.00 | 420,430.00 |
| Mitaji | 15,498.00 | 16,790.00 | 17,151.00 | 22,390.00 | 29,220.00 | 37,115.00 |




Chanzo:Benki ya Watu wa Zanzibar-2010-2015

**Viambatanisho vya Muelekeo wa Bajeti kwa mwaka**

**2015-2016**

**Kiambatanisho namba XVI**

| Mapato yatakayokusanywa na Wizara pamoja na Taasisi zake kwa mwaka 2015/16 | | | |
|---|---|---|---|
| **Maelezo:** | **Makadirio 2014/15** | **Makadirio 2015/16** | **Ongezeko** |
| **Mapato ya Ndani:** | TZS "000,000" | TZS "000,000" | % |
| Bodi ya Mapato(ZRB) | 181,549.60 | 225,943.90 | 24% |
| Mamlaka ya Mapato(TRA) | 166,055.90 | 178,539.70 | 8% |
| PAYE kutoka SMT | 21,000.00 | 21,000.00 | |
| Gawio la Mashirika | 3,200.00 | 5,000.00 | 56% |
| Mapato yasiyokuwa ya kodi | 5,347.50 | 6,882.70 | 29% |
| Mikopo ya ndani | 15,000.00 | 30,000.00 | 100% |
| **Jumla ndogo** | **392,153.00** | **467,366.30** | **19%** |
| Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 266,041.30 | 349,876.10 | 32% |
| **Jumla kuu** | **658,194.30** | **817,242.40** | 24% |

**Kiambatanisho namba XVII**


## Program kuu na ndogo za Wizara zitakazotekelezwa mwaka wa Fedha 2015/2016

| S/N | Program kuu | Program ndogo | Idara itakayosimamia utekelezaji |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 1 | Usimamizi wa Bajeti na fedha za Umma | Mfumo wa Udhibiti na ullipaji | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali |
| | | Usimamizi wa Bajeti ya Serikali | Idara ya Bajeti |
| | | Ufuatiliaji na uratibu wa misaada/mikopo kutoka kwa washirika wa Maendeleo | Idara ya Fedha za Nje |
| 2 | Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma | Usimamizi wa Mitaji ya Umma | Idara ya Uhakikimali na Mitaji ya Umma |
| | | Usimamizi wa manunuzi na uhakiki wa mali za Serikali | |
| 3 | Usimamizi Mfuko Mkuu wa Serikali | Usimamizi Mfuko Mkuu wa Serikali | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali |
| 4 | Mipango na Uendeshaji wa Sekta ya Fedha | Utawala na uendeshaji wa Wizara | Idara ya Utawala na Uendeshaji |
| | | Mipango, Sera na Tafiti za Sekta ya Fedha | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti |
| | | Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | Ofisi kuu -Pemba |

**Kiambatanisho namba XVIII**

| | Makadirio ya Mgao wa Fedha kwa mwaka 2015/2016 kwa Programu | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S/N | Program kuu | Program ndogo | Fedha zinazohitajika | Mgawanyo wa Fedha kiutekelezaji TZS "000,000" | | | |
| | | | TZS "000,000" | Mishahara | Ruzuku | Matumizi mengineyo | Matumizi ya Maendeleo |
| 1 | Usimamizi wa Bajeti na fedha za Umma | | 43,597.32 | 17,919.00 | 21,502.20 | 1,646.12 | 2,530.00 |
| | | Mfumo wa Udhibiti na ullipaji | 26,221.40 | 2,562.30 | 21,502.20 | 1,126.90 | 1,030.00 |
| | | Usimamizi wa Bajeti ya Serikali | 15,588.24 | 15,219.90 | | 368.34 | |
| | | Ufuatiliaji na uratibu wa misaada/mikopo kutoka kwa washirika wa Maendeleo | 1,787.68 | 136.80 | | 150.88 | 1,500.00 |
| 2 | Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma | | 2,250.68 | 335.30 | 250.00 | 165.38 | 1,500.00 |
| | | Usimamizi wa Mitaji ya Umma | 2,151.21 | 335.30 | 250.00 | 65.91 | 1,500.00 |
| | | Usimamizi wa manunuzi na uhakiki | 99.47 | | | 99.47 | |
| 3 | Mipango na Uendeshaji wa Sekta ya Fedha | | 26,351.00 | 1,721.50 | 1,900.00 | 3,229.50 | 19,500.00 |
| | | Utawala na uendeshaji wa Wizara | 5,281.50 | 827.60 | 1,900.00 | 2,553.90 | |
| | | Mipango, Sera na Tafiti za Sekta ya Fedha | 19,831.32 | 122.50 | | 208.82 | 19,500.00 |
| | | Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | 1,238.19 | 771.40 | | 466.79 | |
| 4 | Usimamizi Mfuko Mkuu wa Serikali | | 83,548.70 | 1,300.00 | | 82,248.70 | |
| | | Usimamizi Mfuko Mkuu wa Serikali | 83,548.70 | 1,300.00 | | 82,248.70 | |
| JUMLA KUU | | | 155,747.70 | 21,275.80 | 23,652.20 | 87,289.70 | 23,530.00 |

**Kiambatanisho namba XXI**



**Kiambatanisho namba XX**

Tarakimu ni TZS "000,000"

**Miradi/Programu zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/1**

| S/N | Jina la Mradi/Programu | Wachangiaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Washirika wa Maendeleo | | |
| | | SMZ | Ruzuku | Mkopo | Mshirika |
| 1 | Mradi wa kuimarisha huduma za Jamii Mijini | 1,000.00 | | 18,200.00 | World Bank |
| 2 | Programu ya Usimamizi wa Rasilimali Fedha | 1,500.00 | | | |
| 3 | Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali | 1,500.00 | | | |
| 4 | Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma | 30.00 | 1,000.00 | | Norway |
| 5 | Mradi wa utayarishaji wa Mpango Mkuu wa maeneo huru Fumba | 300.00 | | | |
| **Jumla ya Fedha zinazohitajika** | | **4,330.00** | **1,000.00** | **18,200.00** | |

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe, Mwenyekiti ametaka dakika kumi na tano, kwa hivyo, namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

**Mhe. Hija Hassan Hija (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo):** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na niombe kuwasilisha hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio na Mampato na Matumizi ya Wizara ya Fdha kwa mwaka 2014/2016 na kwa muda ambao

umebakia Mhe. Naibu Spika, nategemeea kumaliza, lakini unaweza ukanipa na dakika tano ili kumalizia hotuba yangu kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, Hatuna budi kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima tukaweza kukutana tena katika Mkutano wa Ishirini kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, Nichukuwe nafasi hii pia kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati wakati wote tulipokuwa tukifanya kazi zetu za kawaida za Kamati. Tunawashukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, Aidha, napenda kuipongeza tena Wizara ya Fedha kwa kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa umahiri na ufanisi mkubwa katika mfumo mpya wa bajeti unaozingatia programu *"Programme Based Budget"(PBB).*

Mhe. Naibu Spika, Sitakuwa nimetenda haki iwapo nitaendelea na hotuba hii bila ya kutoa shukurani za pekee kwa Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati yangu, ambao tumeshirikiana kwa umoja wetu kuyapitia na kuyachambua makadirio haya ya Bajeti ya Wizara hii na hatimae kuyakubali bila ya marekebisho yoyote.

Mhe. Naibu Spika, Kwa kuheshimu, kuthamini na kutambuwa mchango wao mkubwa kwenye Kamati hii hadi kufanikisha kazi hii iliyokusudiwa, naomba niwataje kwa majina Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Hija Hassan Hija | - | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Viwe Khamis Abdalla | - | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Hamad Masoud Hamad | - | Mjumbe |
| 4. Mhe. Raya Suleiman Hamad | - | Mjumbe |
| 5. Mhe. Jaku Hashim Ayoub | - | Mjumbe |
| 6. Mhe. Asha Abdu Haji | - | Mjumbe |
| 7. Ndg. Haji Khatib Haji | - | Katibu |
| 8. Ndg. Fatma Omar Ali | - | Katibu |

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Baraza la Wawakilishi liliidhinishia Wizara ya Fedha Matumizi yenye jumla ya Tshs. 31.786 bilioni kwa ajili ya Fungu 19 kwa Matumizi ya kazi za Kawaida. Aidha, Baraza pia liliidhinishia Wizara ya Fedha Kutumia jumla ya Tshs. 41.5 bilioni kwa ajili ya Matumizi ya kazi za Maendeleo. Vile vile, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya Tshs. 3.20 bilioni kama ni mapato yatokanayo na ukodishwaji/uwekezaji wa mali za Serikali ambapo hadi kufikia Machi, 2015 Wizara ilikuwa imeshakusanya jumla ya Tshs. 3.92 bilioni katika ukodishwaji na uwekezaji wa mali za Serikali ambazo ni sawa na asilimia 123% ya makadirio ya mapato kwa mwaka.

Mhe. Naibu Spika, Kutokana na mafanikio makubwa yaliotokana na jitihada za Wizara ya Fedha zilizopelekea kuongezeka ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia fedha za mitaji iliyoekezwa katika Kampuni na Mashirika. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inapenda kuchukua fursa hii tena kuipongeza Wizara chini ya Mhe. Omar Yussuf Mzee na Katibu Mkuu kwa kuongeza mapato hayo na naomba waendelee kukusanya mapato na kusimamia vyanzo vya mapato hivyo.

Mhe. Naibu Spika, Imeelezwa katika hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya Fedha, kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016, Wizara ya Fedha imepangiwa Tshs. 48.7 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Tshs. 23.53 bilioni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Aidha, inakadiriwa kutumia Tshs. 83.9 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Fungu F02 la Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, katika utaratibu mpya wabajeti inayozingatia programu (*PBB*), Wizara hii imepangiwa kutekeleza Programu Kuu Nne (4) na Programu Ndogo Tisa (9).Kama zilivyofafanuliwa katika hotuba hiyo ya bajeti ya Wizara hii ya Fedha.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu pia inasisitiza Wizara kuwa makini sana na matumizi ya fedha zitakazoingizwa katika Programu hizo kwani licha ya uhaba wa fedha, matokeo ya fedha zitakazoingizwa yatahitaji kuonekana na kupimwa kwa umakini na ufanisi mkubwa hususan katika utekelezaji wa Programu hizo muhimu.

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (*TRA*)**

Mhe. Naibu Spika, Pamoja na utekelezaji mzuri wa majukumu na malengo ya taasisi hii, Kamati inaitaka Mamlaka hii ya Mapato kuzidi kuwa macho na kuandaa mikakati ya kisasa inayokwenda na wakati wa karne hii ya sayansi na teknolojia ili kuweza kudhibiti udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kwa mashirikiano na baadhi ya watendaji wanaoweza kutoa taarifa zisizo za kweli kuhusu aina, wingi na gharama za bidhaa zao wanapoingiza bidhaa hizo hapa nchini kwani kufanya hivyo kunaikosesha sana mapato Serikali ambayo yanahitajika katika shughuli mbali mbali za kimaendeleo hapa nchini. Aidha, Kamati inaitaka Wizara na Mamlaka hii kutochelewa kumchukulia hatua mtendaji

yeyote anaebainika kushiriki au kusababisha udanganyifu na upotevu wa mapato ya Serikali ili kudhibiti kikamilifu nidhamu ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali.
Mhe. Naibu Spika, Sambamba na hilo, Kamati inaitaka Wizara pamoja na Taasisi husika kushirikiana kwa pamoja kuweza kuajiri wataalamu wazalendo wa kusoma mashine ya ukaguzi wa makontena wakati wa kushushwa makontena hayo bandarini ili kuondoa usumbufu wa aina mbali mbali unaotokana na ukosefu wa wataalamu hao. Aidha, tunatanguliza pongezi kwa *TRA* kwa kukubali agizo la Kamati la kuajiri mwanasheria katika Afisi ya *TRA* Zanzibar.

**BODI YA MAPATO (*ZRB*)**

Mhe. Naibu Spika, Nchi yoyote duniani bila ya kukusanya kodi haiwezi kupata maendeleo yoyote, tunapozungumzia maji safi na salama maana yake ni kodi, tunapozungumzia elimu bora nchini maana yake ni kodi na hata tunapozungumzia madawa hospitalini maana yake ni kodi. Kwa maana hiyo huwezi kuzungumzia maendeleo ya nchi bila ya kuhusisha ulipaji wa kodi nchini.

Mhe. Naibu Spika, Kwa kuwa ukusanyaji wa mapato ya visa kwa njia ya mashine hapo uwanja wa ndege wa Zanzibar umeonesha mafanikio makubwa kwa kuweza kukusanya Dola za Marekani milioni 3.2 kwa kipindi cha miezi tisa tu ukilinganisha na Dola 400,000 za hapo kabla, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, inaiomba Serikali pamoja na Wizara ya Fedha kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa kodi za ndani na nje katika maeneo mbali mbali ya vianzio vya mapato kwa kutumia machine za elekroniki na kuachana na mfumo wa kizamani uliopitwa na wakati wa ukusanyaji wa kodi kwa njia ya mkono, kwani kutumika kwa mfumo huo wa kizamani ni kuendelea kuiokosesha nchi mapato yake yanayostahiki hasa kwa kuwa fedha nyingi za Serikali huwa zinavuja na kuingia katika mifuko ya wachache tu.

Mhe. Naibu Spika, Kwa hiyo, Kamati inaiagiza Wizara na vyombo vyake vyote kuhakikisha maeneo yote ya vianzio vya mapato, mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa mkono (*cash*) iwe mwisho ifikapo Juni 30, 2015 na sasa tutumie *Visa Card* kwa lengo la kudhibiti mapato. Ukweli Kamati inauhakika wa upotevu wamapato katika maeneo mengi yakiwemo Viwanja vya Ndege, Bandari, Mji Mkongwe, kwenye mbuga, maeneo ya Historia, Bahari kuu n.k. Kamati pia inaamini iwapo utaratibu mzuri utawekwa katika maeneo hayo mapato ya nchi yataongezeka mara dufu na matokeo yake tutapunguza utegemezi wa bajeti zetu na kukuza maendeleo ya Taifa.

**SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR**
Mhe. Naibu Spika, Kama inavyofahamika kuwa Shirika la Bima la Zanzibar lina jukumu la kutoa huduma za Bima kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, Lisha ya mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika Shirika hili, bado maslahi madogo kwa watendaji wake imeendelea kuwa ni changamoto sugu ya Shirika hili. Hivyo, Kamati inamuomba na kumtaka Mheshimiwa Waziri Fedha kaka yangu Omar Yussuf Mzee, atakapokuja hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuja kufanya majumuisho atupatie maelezo ya kina juu ya hatua zilizofikiwa kuhusiana na maslahi ya watendaji wa Shirika la Bima.

**PROGRAMU NDOGO YA UFUATILIAJI NA URATIBU WA MISAADA KUTOKA KWA WASHIRIKA WA MAENDELEO**

Mhe. Naibu Spika, Sote ni mashahidi juu ya namna ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2014/2015 ilivyoathirika kutokana na kuzuiwa kwa misaada ya kibajeti na Washirika wa Maendeleo kulikotokana na sakata la *Escrow Account*. Hivyo, Kamati inatoa indhari tu juu ya Wizara kuongeza umakini na kutoa uelewa mzuri juu ya Wahisani wetu juu ya masuala mbali mbali yanayohusu Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ikiwemo mfumo na muundo wa kisiasa, kiutawala, kiuchumi na kijamii uliopo hapa nchini ili misaada hiyo ipatikane kwa uhakika wakati jitihada za kukuza mapato ya vianzio vya ndani zikiendelea.

Mhe. Naibu Spika, Aidha, Kamati ilipatwa na butwaa juu ya kauli zinazogongana juu ya fedha za misaada ya kibajeti (*GBS*) zilizopatikana hapa Zanzibar kwa kipindi cha miezi 9, Wizara ya Fedha ilituambia ni Tshs. 7.5 bilioni tu ndizo zilizopatikana, lakini Benki Kuu (*BOT*) waliiambia Kamati kuwa ni zaidi ya Tshs. 24 bilioni ambazo ni asilimia 80% ya *GBS* iliyopatikana kipindi hicho.

**Programu Ndogo ya Uratibu wa Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba**

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaitaka Wizara ya Fedha kuwa makini katika utekelezaji na usimamizi wa uratibu wa shughuli za Wizara kwa Pemba kwani Kamati inaona kuwa kuna baadhi ya masuala ya usimamizi hauendi inavyostahiki. Kwa mfano, Wizara ya Fedha Pemba ina akaunti maalum kwa ajili ya fedha za maendeleo, akaunti ambayo ingeweza kutumiwa na Wizara mbali mbali kwa ajili ya fedha za kazi za maendeleo zinazotekelezwa kwa upande wa Pemba. Hata hivyo, akaunti hiyo inaonekana kukaa bure na kutotumika ipasavyo na taasisi za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, aidha, Kamati imegundua kuwa Wizara ya Fedha Pemba inatumia utaratibu wa Divisheni badala ya Idara. Hivyo, ni wakati muafaka sasa Serikali kwa ujumla kuwa na mfumo na muundo wa Wizara Pemba unaofanana.

Mhe. Naibu Spika, idhini ya mapato na matumizi ya fedha kwa Wizara hii imeshaombwa mbele ya Baraza lako Tukufu hivi punde. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo iliyapitia na hatimae kuyakubali mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016,

na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wako waijadili, watoe mapendekezo yao na hatimae kuipitisha Bajeti hii. Mhe. Naibu Spika, wakati Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe waijadili na hatimae waipitishe bajeti ya Wizara ya Fedha, Kamati ingependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe na Taifa kwa ujumla kuwa historia inaonyesha miradi mingi mikubwa hapa Zanzibar imekuwa ikikumbwa na changamoto nyingi na nzito.

Mhe. Naibu Spika, changamoto hizo husababishwa na mambo mengi miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na:-

1. Ukiukwaji wa Sheria na Kanuni za Fedha.
2. Uwajibikaji mbovu.
3. Ushirikishwaji mdogo wa wataalamu wa ndani.
4. Ubinafsi wa baadhi ya watendaji.
5. Uwezo mdogo wa Wakandarasi.
6. Mikataba inayotoa fursa ya kuitia nchi hasara.
7. Fedha ndogo.
8. Kukosa uwezo wa ndani wa kifedha wa kutekeleza miradi hiyo, n.k.

Mhe. Naibu Spika, sababu hizi na nyenginezo zimekuwa kwa kiasi kikubwa zikidhoofisha utekelezaji wa miradi mingi ya Zanzibar, na maana yake inapofeli au kutofikia malengo kwa wakati, maana yake ni kilitia Taifa hasara na kuwabebesha mzigo wa madeni wananchi maana baadhi ya fedha za miradi hii ni mikopo.

Mhe. Naibu Spika, wakati Kamati inatoa hoja hii, nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe baadhi ya miradi iliyotumia fedha nyingi na kuwa na ufanisi mdogo.

1. Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Abiria *(Terminal II)* Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar;
2. Mradi wa Maji Mkoa wa Mjini Magharibi;
3. Mradi wa Huduma za Miji na Vijiji (*ZUSP*);
4. Miradi ya Barabara za Kaskazini Pemba;
5. Mradi wa Soko la Samaki Zanzibar;
6. Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Afisi ya Wizara ya Fedha Pemba;
7. Mradi wa Barabara 6 za Kusini Pemba;
8. Mradi wa Barabara ya Ole Kengeja;
9. Mradi *E- Government*;
10. Mradi wa Uwekaji wa Taa Barabarani;
11. Mradi wa Uwekaji wa Camera za Ulinzi (*CCTV – CAMERA*); na
12. Mradi wa Ujenzi wa Skuli 10 za Sekondari za Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, miradi hii 12 kwa kweli imeitia nchi hasara na haikufanikiwa kiufanisi unaotakiwa. Miradi mingi mengineo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wanaijua, yote haya yana masuala mengi na yanahitaji majibu kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, Kamati haikusudii kutonesha vidonda ila lengo ni kujikumbusha tunakotoka, maana mwanaadamu hutakiwa ajifunze na makosa ili tulipofika tusije tukaendelea napo tena.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii na katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani tukiwa katika Kumi la Mwanzo Kumi la Rehema.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, nikiwa kama Mwakilishi wa Jimbo la Kiwani na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, naomba unipe dakika tano ili niweze kutoa mchango wa jumla kwa niaba ya wananchi wangu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru sana Mhe. Omar Yusuf Mzee kama Waziri wa Fedha, nimshukuru pia Katibu Mkuu na watendaji wake wote, kwa jinsi ambavyo Kamati yetu wameipa mashirikiano muda wote tangu uhai wa Mhe. Salmin Awadh, nikiwa Makamo Mwenyekiti, na sasa nikiwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, hatujawahi kupata changamoto yoyote kwenye Wizara hii ya kiutendaji, kila ambalo Kamati walilihitaji kulijua walifanya kazi hiyo, walitusaidia hata kwenda kuhoji masuala ya fedha kule Tanzania Bara (*BOT*) Kamati yetu iliwezeshwa na wizara hii na tukaenda bila ya kificho.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hiyo kwa dhati kabisa ikiwa hii ni bajeti ya mwisho napenda kuwapongeza sana wenzetu hawa wa Wizara ya Fedha na kwenye Kumi hili la Maghfira nadhani tuombe mwakani baada ya uchaguzi Mhe. Spika, atuchague tena tuwe kwenye Kamati ya Fedha ili ile kazi nzuri iweze kuendelea na viongozi wetu wa Wizara ya Fedha iyende kwa ufanisi mkubwa.
Mhe. Naibu Spika, lakini pia niwapongeze Makatibu wangu wa Kamati kwa kweli Makatibu wangu wa Kamati ni watiifu sana, walikuwa wanafanya kazi zaidi ya maagizo ya Kamati. Muda wote wa miaka miwili na nusu hatukupata mgongano wowote na makatibu wetu, walikuwa watiifu na kwa kweli niwashukuru kwa niaba ya Katibu wa Baraza kwamba walikuwa ni makatibu wazuri.

Mhe. Naibu Spika, lakini jambo la pili kwa niaba ya Kamati nitoe masikitiko kwamba Kamati yetu ilikuwa ina shida ya kufanya mkutano na *TRA* pamoja na *ZRB* chini ya usimamizi wa Kamati na Wizara ya Fedha. Kamati yangu ilihangaika

sana zaidi ya miezi miwili kuomba mkutano huo wa *TRA* na *ZRB* pamoja na *Chamber of Commence*. Lengo lilikuwa ni moja tu ni kubadilishana mawazo juu ya upotevu wa fedha za umma. Kamati yangu ilikuwa ina lengo la kuonyesha watendaji hawa jinsi fedha inavyotafunwa, yaani fedha ya nchi. Kwa bahati mbaya jitihada zote zile za Kamati hatukufanikiwa kwa miezi miwili mfululizo.

Kwangu mimi kama Mwenyekiti wa Kamati tafsiri yangu ni kwamba walikuwa wanakwepa. Sasa hili si jambo zuri, unapokuwa na Wawakilishi wanakuonyesha kwamba hii njia ambayo si nzuri, fedha inapotea wewe ukawa unawakwepa hutaki kuwasikiliza maana yake unaonyesha sura mbaya. Nimuombe kaka angu Mhe. Waziri, hili limepita na limetendeka na nikuombe mwakani tukijaaliwa baada ya uchaguzi basi jambo hili Wajumbe watakaokuwa kwenye Kamati ya Fedha kuwasikiliza kwa ajili ya kuongeza nguvu ya kasi ya mapato ya nchi ya Zanzibar.
Mhe. Naibu Spika, Kamati pia inaomba sana kumuomba Kamishna wa *TRA* na *ZRB* waendelee kusimamia mapato ya nchi kwa sababu bila ya mapato hatuwezi kujenga nchi, bila ya mapato hatuwezi kutekeleza miradi ya serikali na wananchi kwa jumla. Ile mianya ambayo tumeigundua wakati wote wa Kamati mimi niombe kwamba sisi hatuhitaji mtu kufungwa, lakini lengo letu ni kuhitaji nidhamu ya fedha ipatikane kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Hoja ya tatu ambayo naomba nichangie kwa haraka haraka ni hoja ya Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Fedha Pemba ambalo hili limezungumzwa miaka mingi. Nilikuwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati Teule ya kuchunguza jengo lile la Pemba ambalo lilifeli na tukawambia serikali kwamba hakuna hoja ya *habituation. Habituation* serikali itashindwa tu kwa sababu pale uzeme ulifanyika wa serikali. Sasa mnaendea kwenye mradi mpya wa ujenzi wa Ofisi, nimuombe kaka yangu Mhe. Omar Yussuf Mzee na Katibu Mkuu mara hii wawe makini, wasiwaamini watu, sio kila mtu anaaminika, msimamie wenyewe ili majengo yaweze kupatikana kwa ufanisi uliokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa niwashukuru sana wananchi wa jimbo la Kiwani kwa jinsi walivyonivumilia na ndio maana mara hii kwa sababu waliniamini wakanipa kura nyingi sana kwa asilimia 73 ya kura za jimbo. *(Makofi)* Na penye uhai *Inshaallah* nategemea kurudi tena nikiwa Mwakilishi. Niwaombe wanivumilie waniunge mkono, nilikuwa mkali sana Barazani, lakini sikuwahi kugongana na mtu. Kwa hivyo, Mawaziri wote ambao kuwa nilikuwa nikiwachora kwa namna moja au nyengine waone kuwa ni wajibu wangu wa kazi na sikuwa na nia mbaya, leo ni marafiki, leo tupo pamoja na nawaheshimu na nitawaheshimu kwa sababu penye kazi hakuna udugu lazima tuwajibike.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru na naomba kuwasilisha hoja yangu hiyo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha hoja ya Kamati na mchango wako tunakushukuru. Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha nina tangazo moja.

Katibu wa Baraza la Wawakilishi anawatangazia Kamati ya Uongozi kwamba kile kikao kilichokuwa kifanyike saa 8:00 ukumbi wa juu kimeakhirika mpaka litolewe tangazo jengine.

Baada ya hayo Wajumbe nawashukuru kwa ushirikiano wenu mzuri nakuweza kupitisha bajeti yetu ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, tunampongeza Waziri na watendaji wake wote. Baada ya maelezo hayo naakhirisha kikao chetu hichi hadi siku ya Jumatatu tarehe 22/06/2015, saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 5:52 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 22/06/2015 saa 3:00 asubuhi)*